**MAJIBU** ya DNA padri anayeshtakiwa kubaka sasa tayari

UKURASA 4



**LHRC** yapendekeza mchakato mabadiliko ya sheria kandamizi

UKURASA 4



ama

AFYA NA MAZINGIRA

Mkoa Manyara unavyong'ara katika operesheni chanjo wajawazito, watoto

Unajua msamaha unakuepusha na milolongo wa maradhi mwilini?

**Hospitali rufani zote kupata huduma dharura na mitungi mikubwa ya gesi**

Bomba hadi wodini, zahanati kunufaika

UKURASA 11


# Nipashe

Alhamisi Mei 6, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0580572

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710


# MAHINDI RUKSA KENYA


**NI** yaliyokwama mpakani, Kenyatta ataka yaondolewe mara moja, Rais Samia asema uhasama sasa basi...*Endelea Ukurasa 2*




Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia mabunge mawili ya Jamhuri ya Kenya, la Seneti na Taifa, jijini Nairobi jana. **PICHA: IKULU**

# NHIF yatekeleza agizo la Rais

UKURASA 3



UKURASA WA 5

**KILICHOMUUA TEDDY MAPUNDA**

MJASIRIAMALI na mdau wa vyombo vya habari, Teddy Mapunda, amefariki dunia baada ya kuugua ghafla wakati...

**Mwanafunzi adaiwa kujitoa ujauzito kwa kijiti**

UKURASA 3

**MICHEZO** GOMES: HESABU KAIZER CHIEFS CAF KWA YANGA UK. 24

MAONI, KATUNI UK. 6

## ... Ateta na mwakilishi wa Katibu Mkuu UN

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana alikutana na kufanya mazungumzo na Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN) katika Ukanda wa Maziwa Makuu, Balozi Xia Huang, jijini Nairobi.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa, ilisema katika mazungumzo hayo, Balozi Huang aliwasilisha salamu za pole za Katibu Mkuu wa UN, António Guterres, kwa Rais Samia kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli.

Sambamba na hilo, aliwasilisha pongezi kwa Rais Samia kupokea kijiti cha urais akiwa mwanamke wa kwanza kuwa Rais nchini Tanzania.

Balozi Huang alisema UN inayo matumaini makubwa na uongozi wa Rais Samia katika kuiongoza Tanzania na kuendeleza ajenda za ukanda wa maziwa makuu ambazo ni kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi na pia kuendeleza juhudi za kulinda amani na kuimarisha usalama.

Taarifa ilisema ameipongeza Tanzania kwa mchango na ushirikiano mkubwa inaoutoa kwa UN katika juhudi za kulinda amani na kuimarisha usalama katika maeneo yote yenye mapigano na makundi yanayohasimiana na ameahidi kuwa umoja huo utaendelea kushirikiana na Tanzania kulinda amani ili maendeleo ya jamii na uchumi yastawi.

Rais Samia, taarifa hiyo ilisema amepokea salamu za pole na pongezi kutoka kwa Guterres na amemhakikishia kuwa serikali itaendelea kushirikiana na umoja huo katika juhudi za kulinda amani na usalama katika Maziwa Makuu.

Samia alisema hali ya ulinzi na usalama na demokrasia nchini Tanzania ni nzuri na ameomba UN kuendeleza jitihada za kulinda amani na usalama katika maeneo yote yenye matatizo.

Aidha, Rais Samia alitoa wito kwa umoja huo kuushawishi Umoja wa Ulaya (EU) kuondoa vikwazo vya kiuchumi dhidi ya Burundi.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza wakati akizindua kampeni za CCM za uchaguzi mdogo wa Jimbo la Buhigwe, katika Uwanja wa Shule ya Msingi Buhigwe, mkoani Kigoma, jana. **PICHA: OWM**

# Mahindi ya Tanzania ruksa Kenya

**Na Christina Mwakangale**

RAIS wa Kenya, Uhuru Kenyatta ameagiza kufunguliwa mara moja kwa bidhaa zilizozuiwa, yakiwamo mahindi, katika mpaka wa Kenya na Tanzania ndani ya saa 24 ili kuondoa msongamano wa bidhaa zilizokwama.

Rais Kenyatta alitoa agizo hilo jana jijini Nairobi, mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, walipohudhuria kongamano la wafanyabiashara wa nchi hizo mbili na kushirikisha wadau wa sekta hiyo wakiwamo maofisa wa serikali na binafsi na mabalozi.

"Ninataka mkutane wiki hii, mkatatue matatizo ya Namanga na magari yapite. Mwondoe vikwazo vya vyeti kuhusu corona. Ili watu wafanye biashara.

"Siku mbili zilizopita tumesikia kuhusu nchi zetu mbili katika kukuza maslahi ya Watanzania na Wakenya na nina imani kwamba Rais Samia ataendelea kuimarisha uhusiano huu.

"Nina imani tuna mahitaji yanayofanana na lengo ni kukuza biashara. Kenya na Tanzania tunafurahia kuwa tuko pamoja katika kilimo, biashara, viwanda, dawa na biashara kwa ujumla. Tukiwa kama waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), tumeendelea kufanya kazi pamoja kuimarisha umoja huu," alisema.

Alibainisha kero zilizopo kwenye biashara ambazo zinahitaji kuchukuliwa hatua, zifanyike mara moja ili kutumia fursa ya biashara huru katika ukanda wa EAC.

"Kufanya kazi pamoja kunaweza kuinua uchumi wa Tanzania na Kenya tuna nia ya kuhakikisha tukifanya pamoja tutasonga mbele," alisema Rais Kenyatta na kuongeza kuwa nchi hizo mbili hazina haja ya kushindana badala yake zishirikiane kwa sababu siku zote nchi zinazoshindana hushindwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa na kufikia maendeleo.

"Tukishindana tutashindwa kuwa na viwanda ambavyo vinatakiwa kurithiwa na vijana wetu na tutabakia kununua bidhaa kutoka nje. Tununue bidhaa ambazo zimetengenezwa kwenye nchi zetu na vijana itakuwa ajira kwao.

"Isiwe tu tunatoa malighafi kwenda viwanda vya nje. Nakumbuka umetukumbusha Kenya ni taifa la tano kuwekeza Tanzania pia. Sisi tungependa kuona wawekezaji wengi zaidi nchini wafanye kazi, sitangoja waziri aseme nasema mwenyewe," alisema.

BIASHARA BILA VIBALI

Rais Kenyatta alisema katika kuimarisha shughuli za kiuchumi kwa nchi hizo mbili, hivi sasa biashara zitapita mipakani bila kusubiri utaratibu wa vibali maalum ikiwamo vya kazi.

"Watanzania wapo huru kuwekeza Kenya bila vibali vya kazi, inatakiwa kufuata sheria kama ilivyo kwenu zinavyofuata. Tumerahisisha njia za kufanya biashara Kenya. Suala la kusubiri mawaziri mkutane hadi wiki zipite haifai. Mkutane na kuamua kutatua shida za wananchi wetu," alisisitiza.

Kenyatta alisema kwa pamoja na mwenzake (Samia), wamekubaliana kutatua changamoto za wafanyabiashara na kutekeleza maagizo haya kama ilivyoelekezwa na mawaziri kwenye mkutano huo.

Rais Samia alisema Tanzania iko tayari kuwapokea wawekezaji kutoka Kenya na kwamba serikali yake imechukua hatua ya kuleta mageuzi ili kufanya mazingira ya kufanyia biashara kuwavutia wawekezaji kutoka Kenya kwa lengo la kutumia fursa zilizopo.

Alisema Tanzania ina ardhi, vivutio vya utalii na rasilimali ambazo zinaweza kutumiwa kuboresha hali ya kiuchumi wa mataifa yote mawili. Pia alisema sekta binafsi ni nguzo muhimu ya kuhakikisha kwamba nafasi za ajira zipo kwa wananchi wa mataifa yote.

"Tunaishi katika dunia ya kutegemeana hakuna ambaye anaweza kufanikiwa pekee yake. Biashara na maeneo yanaweza kuwa msaada mzuri na ushirikiano huu unaweza kubadili maisha ya wananchi wetu," alisema.

"Ili kuwe na ongezeko la ajira, ujasiriamali inatakiwa kujengwa na serikali zetu ili mazingira hayo yasaidie sekta binafsi. Tanzania imeendelea kujenga mazingira ya uwezeshaji, mfano kupunguza makato ya kodi, kupambana na rushwa, matumizi ya ardhi na kuondoa vikwazo vya kibiashara," aliongeza.

# Samia: Udugu daima, uhasama hauna nafasi

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema Tanzania na Kenya imeamua kujenga utamaduni wa kukutana mara kwa mara kujenga udugu zaidi na kwamba uhasama hauna nafasi katika nchi hizo.

Amesema amepewa heshima kubwa kulihutubia Bunge la Jamhuri ya Kenya na Seneti na kuweka historia kwenye uongozi wake katika nyakati za mwanzo.

Rais Samia alitoa kauli hiyo wakati akihutubia mabunge hayo na kwamba Rais Uhuru Kenyatta alimtumia mwaliko wa barua ili kufika Kenya, ikiwamo salamu za pole kufuatia kifo cha Rais Hayati John Magufuli, aliyefariki, Machi 17, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Alisema wakati wa mazungumzo na Rais Kenyatta alisema ili kufikia muafaka katika masuala ambayo yanaleta tofauti ikiwamo kukwama kwa biashara mipakani, yamefikia hatua ya maafikiano.

Alisema kutokana na uhusiano uliopo katika shughuli za kijamii, kiuchumi kwa nchi hizo mbili hazitatoa nafasi ya uhasama au mifarakano.

"Ili kuondoa mitazamo hasi kati yetu tumeamua kujenga utamaduni kwa kukutana mara kwa mara, ndugu wanaotembeleana hujenga udugu zaidi. Uhasama hauna nafasi.

"Hii ziara yangu ya kwanza nchini Kenya nikiwa rais, na itaweka historia ya rais awamu ya sita kufika Kenya. Uganda ilikuwa si ziara rasmi hii hapa Kenya nimealikwa rasmi."

Rais Samia alisema ameanzia Kenya kwanza kutokana na uhusiano uliopo kihistoria licha ya kuwa Tanzania inapakana na nchi nane.

"Kabla hata ya uhuru, jiografia imetufanya tuwe na uhusiano. Ushirika na ujirani unatufanya kwa pamoja, tunategemeana kila hali, neema au dhiki.

Njaa ikitokea Kenya na Tanzania inapiga hodi tupakane na tuelewane kwa pamoja. Nashangaa wale ambao wanaodhani kuwa Kenya pekee inaweza kuendelea bila mwenzake," alisisitiza Rais Samia.

Pia alisisitiza serikali yake kuendelea kutoa ushirikiano, na kuwaalika Wakenya zaidi kuja kuwekeza Tanzania.

"Tuna rasilimali za kutosha, ardhi, madini, tunakosa mtaji. Kenya mna mtaji wa kutosha. Pia tuzungumze namna ambayo Tanzania pia itawekeza Kenya.

"Bidhaa za usafirishaji zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 390.7 mwaka 2017 hadi bilioni 500 mwaka 2020.

"Viongozi tuanze kubadilika, mimi na Kenyatta tumeamua kuondoa tatizo kwenye mipaka yetu, ikolojia zinaingiliana ikiwamo utalii, hivyo tunaweza kuneemeka pamoja pasipo kushindana."

Rais Samia alisema ujenzi wa miradi kadhaa ikiwamo ya miundombinu ya barabara za lami kutoka Lamu, Tanga, Bagamoyo, yenye urefu wa kilomita 454 iliyo chini ya mpango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), imefikia pazuri.

"Mradi wa vituo vya pamoja mipakani umerahisisha biashara mipakani, kwa kuinua uchumi na Lungalunga, Silali, Holoholo ili vitoe huduma kirahisi."

Kuhusu corona, Rais Samia alisema imesababisha kuporomoka uchumi duniani na kwamba nchi hizo mbili zimeweka mikakati ya kukabiliana na Covid-19.

"Tanzania sio kisiwa tunaishi kama sehemu ya jumuiya ya dunia, nimeunda tume ili kufanya utafiti kuhusu ugonjwa wa corona, tukisubiri mapendekezo ya wataalamu, lakini hatuwezi kuacha kushirikiana, japokuwa kuna janga la corona haiwezi kutufarakanisha," alisema Rais Samia.

HABARI KITAIFA

# Bima ya Afya yatekeleza maagizo ya Rais Samia

**Na Romana Mallya**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umesema umeanza utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, ya kuongeza umri wa utegemezi kwenye bima ya afya kutoka miaka 18 hadi 21.

Katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani Jumamosi mkoani Mwanza, Rais Samia aliagiza suala hilo lifanyiwe marekebisho na kueleza kusudio la serikali la kujumuisha uamuzi huo kwenye marekebisho ya sheria ya bima ya afya.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana Meneja Uhusiano wa mfuko huo, Angela Mziray, NHIF imewataarifu wanachama wake kuwa imepokea maelekezo hayo na imeanza kuyafanyia kazi.

"Mfuko umeanza kulifanyia kazi kwa kukamilisha taratibu za ndani ikiwa ni pamoja na mifuko wakati mchakato wa marekebisho hayo ya sheria yakiendelea," ilieleza.

Mziray alisema mfuko huo utatoa taarifa rasmi kwa wanachama na umma kuhusu utekelezaji wa suala hilo.

Katika taarifa hiyo NHIF imewaomba wanachama wake kuendelea kupata huduma katika ofisi zake zilizopo kila mkoa na endapo kutakuwa na uhitaji wa taarifa wasisite kuwasiliana nao.



Mafundi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Andrew Kamanga (katikati) na Jonathan Nkumbi, wakifungulia maji ili wananchi wakinge wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji ya bomba kutoka Ziwa Victoria, katika Kijiji cha Bukima, Wilaya ya Musoma mkoani Mara, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwanafunzi adaiwa kujitoa ujauzito kwa kijiti

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI anayesoma kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Uzogole Manispaa ya Shinyanga (jina limehifadhiwa), amedaiwa kujitoa ujauzito kwa kijichokonoa na kijiti, ili aendelee na masomo.

Imeelezwa mwanafunzi huyo alipata ujauzito huo wakati akiwa nyumbani akisubiri matokeo ya kidato cha kwanza, na alipofaulu akaingia nao sekondari, ndipo Januari mwaka huu akaona autoe ili asifukuzwe shule.

Askari Polisi Kata wa Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga ilipo shule hiyo, Emmanuel Maganjila, ilibainisha hayo juzi kwenye kikao cha kujadiliana kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia kwenye kata hiyo, kilichoandaliwa na Shirika la YWCA.

Alisema mwanafunzi huyo alifanikiwa kujitoa ujauzito huo, na kwamba kilitoka kiumbe kikiwa kimekufa, lakini mwanafunzi huyo aliwahishwa hospitali kwa ajili ya matibabu, na sasa anaendelea na masomo.

"Natoa wito kwa wazazi mkoani Shinyanga vunjeni ukimya, zungumzeni na watoto wenu na kuwapatia elimu ya makuzi na madhara ya kufanya ngono katika umri mdogo," alisema Maganjila.

Naye Katibu wa Shirika la YWCA, Marysiana Makundi, ambao wanatekeleza mradi wa kutokomeza ukatili wa kijinsia kwenye Kata ya Ibadakuli, alisema matatizo hayo ya mimba za utotoni ili kuisha, inapaswa wahusika wawe wanafungwa jela badala ya kuachiwa huru.

Alisema mbali na utoaji wa elimu ya kutokomeza matukio ya ukatili wa kijinsia, wazazi wamekuwa kikwazo, kutokana na kuwa na tabia ya kumaliza kesi kimya kimya na watuhumiwa ambao huwapatia ujauzito wanafunzi, kwa kupeana fedha ama mifugo na kusababisha kesi kufutwa mahakamani kutokana na kukosekana ushahidi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Ibadakuli, Mwijage Patrick, aliwataka wazazi mkoani Shinyanga, waachane na mila kandamizi, ambazo zimekuwa zikimnyima haki mtoto wa kike, kwa kuonekana hastahili masomo bali ni wa kuolewa tu, na ndio chanzo cha mimba na ndoa za utotoni kuendelea kwa kasi mkoani humo.

# Wabunge wataka ushirikishwaji wa mabadiliko mitaala

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wametaka kuwapo na ushirikishwaji wa makundi muhimu ya wadau wa elimu kujifunza kutoka mataifa mengine kabla ya hatua ya serikali ya kufanya mapitio katika mitaala ya elimu pamoja na sera ya elimu na mafunzo.

Pia wamesema mapitio hayo yawashirikishe wataalamu na yalenge kutatua tatizo la ukosefu wa ajira nchini, kumwezesha mhitimu wa chuo kikuu, sekondari ama msingi kujiajiri ama kupata kazi.

Waliyasema hayo jana wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mbunge wa Buchosa (CCM), Erick Shigongo, alisema mtaala wa elimu pamoja na sera ya elimu inapaswa kuwajenga wanafunzi kuwa wajasiriamali na wazalendo kwa taifa lao.

Alisema pia wanafunzi wanapaswa kufundishwa kompyuta tangu wakiwa darasa la kwanza, pamoja na maamuzi ya lugha ya kufundishia uwekwe bayana.

Alisema pia elimu itakayotolewa inapaswa ijielekeze katika vitendo zaidi kuliko nadharia, vitendo iwe asilimia 70, nadharia 30.

Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, alisema uamuzi wa serikali kufanyia marekebisho mitaala ya elimu ni mzuri, lakini kilio kikubwa kwa wahitimu ni mfumo wa elimu kushindwa kukidhi mahitaji pindi wanapomaliza masomo.

Alisema pia yanahitajika maandalizi makubwa ya walimu na wakufunzi ili kufanikisha utekelezaji, kwamba kutokufanya hivyo utaishia kwenye wizara ya baadhi ya kanda.

Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Lemburis, alisema mtaala wa elimu unapaswa kueleza lugha inayopaswa kufundishia kuanzia elimu ya awali hadi darasa la saba. Alisema hivi sasa lugha inayotumika kufundishia kuanzia elimu ya awali hadi darasa la saba ni Kiswahili, lakini mwanafunzi akiingia sekondari anafundishwa kwa lugha ya Kiingereza, hali inayowasababisha baadhi ya wanafunzi kuichukia shule. Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Tunza Malapo, alisema: "Mapitio ya mitaala ifanywe kwa utulivu, ishirikishe wataalamu, tatizo elimu yetu inaharibiwa na wanasiasa. Ubadilishaji wa mitaala usiwe wa siku moja, kunapaswa kuwe na maandalizi."

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko, alisema mabadiliko ya mitaala na sera ya elimu yanayokwenda kufanyika yalenge kuwaandaa wanafunzi tangu wakiwa darasa la kwanza.

Mbunge wa Busokelo (CCM), Atupele Mwakibete alisema: "Serikali inapaswa kwenda kujifunza Afrika Kusini, wenzetu wanamfumo unaitwa 'Youth Education System' ambao wahitimu wa vyuo vikuu wanaunganishwa na taasisi na mashirika pindi wanapomaliza masomo."

Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya, alisema: "Nimepitia mfumo wa elimu wa Tanzania, Japan, Marekani, Kenya, China, Uingereza, nilichogundua kuna utofauti wa umri kwa mwanafunzi kujiunga darasa la kwanza."

Dk. Chaya alisema kunapaswa kuwapo na muda wa kutosha katika kupitia mitaala.

Alisema mapitio ya sera ya elimu ni muhimu, lakini serikali inapaswa kuangalia na elimu ya Zanzibar kwa sababu wao elimu ya msingi inaishia darasa la sita.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, alisema mtaala mpya utakaoundwa uwajenge wanafunzi waweze kujiajiri pindi wanapomaliza elimu ya juu.

# Majibu DNA padri anayedaiwa kubaka tayari

**Na Daniel Sabuni,** HAI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, imeelezwa kuwa majibu ya vipimo vya sampuli za vinasaba (DNA) vya aliyekuwa Paroko wa Kanisa Katoliki, Jimbo la Moshi, Erasmus Swai (44), anayekabiliwa na kesi ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne, yako tayari. Padri Swai, kabla ya kushtakiwa kwa kesi hiyo, alikuwa Paroko wa Parokia ya Manushi.

Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Lobulu Mbise, mbele ya Hakimu Mkazi Thurston Kombe, anayesikiliza kesi hiyo Na. 6 ya mwaka 2021, alidai kwamba majibu ya DNA yaliyokuwa yanasubiriwa yako tayari na upelelezi wake umekamilika.

"Mheshimiwa Hakimu, majibu hayo ya DNA yatatolewa hapa mahakamani Mei 12, mwaka huu. Hapo ndipo tutakapojua mwelekeo wa kesi pamoja na idadi ya mashahidi wa upande wa mashtaka wanaoijenga kesi hii," alisema Mbise. Baada ya maelezo hayo kutolewa, Hakimu Kombe, aliahirisha shauri hilo hadi Mei 12 mwaka huu, atakapoanza kusikiliza ushahidi wa mashahidi wa upande wa mashtaka.

Sampuli hizo zilichukuliwa miezi miwili iliyopita kutokana na amri ya mahakama. Padri Swai anadaiwa kutenda makosa hayo kwa mtoto mwenye umri wa miaka 17, ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kimaseki iliyoko mkoani Arusha.

Katika hati ya mashtaka, inadaiwa kuwa Machi, mwaka jana, katika Hoteli ya Snow View iliyoko Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bomang'ombe, kwa nyakati tofauti, Padri Swai alimbaka mwanafunzi huyo.

Iliendelea kudaiwa mahakamani hapo kuwa mshtakiwa alitenda makosa mawili, la kwanza ni kubaka chini ya kifungu cha 130 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 2002 na la pili ni kumpa mwanafunzi ujauzito, chini ya kifungu cha 60 (a) cha Sheria za Elimu.



Magari yakipita kwa tahadhari kutokana na ubovu wa barabara katika makutano ya Mtaa wa Uhuru na Bibi Titi Mohamed, eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# LHRC yapendekeza marekebisho sheria kandamizi

**Na Romana Mallya**

KITUO cha Sheria na Kutetea Haki za Binadamu (LHRC), kimeiomba Wizara ya Katiba na Sheria kuanzisha mchakato wa kufanyia marekebisho sheria zote zinazominya uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Haki za Binadamu mwaka 2020, uhuru wa kujieleza ulidorora katika kipindi cha mwaka huo kwa sababu mbalimbali zikiwamo za utekelezaji wa sheria zinazouminya.

Kwa upande wa uhuru wa kujumuika ripoti hiyo ilisema kuwa pia umedorora na masuala makuu yanayoathiri ufurahiaji ni utekelezaji wa sheria zinazouminya.

Kuhusu mauaji ya wanawake yanayofanywa na wenza wao au wa zamani, ripoti hiyo ilitaja kwa mwaka 2019 jumla ya matukio iliyoyakusanya yalikuwa ni 12 na manane yalihusishwa na wivu wa mapenzi.

"LHRC ilikusanya matukio 32 ya mauaji ya wanawake yaliyofanywa na wenza wao, ambapo matukio 23 yalisababishwa na wivu wa kimapenzi. Matukio haya yanakiuka uhuru wao dhidi ya ukatili pamoja na haki ya kuishi," ilisema ripoti hiyo.

Pia, ilipendekeza Wizara ya Katiba na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kupeleka bungeni muswada wa kutunga sheria maalum dhidi ya ukatili wa kijinsia.

"Wizara ya Fedha na Mipango, kuongeza bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya wanawake na watoto, ikizingatiwa kwamba matukio ya ukatili katika kundi hilo yanaongezeka.

Pia ripoti hiyo ilitaka makundi hayo yatoe taarifa kuhusu matukio ya ukatili wanayofanyiwa na kutoa ushirikiano kwa mamlaka husika ili sheria zichukue mkondo wake.

Kadhalika, ilipendekeza Jeshi la Polisi na mhimili wa mahakama kuongeza kasi ya uchunguzi na uendeshaji wa kesi za ukatili dhidi ya watoto. "Jeshi la Polisi lihakikishe maofisa wake wanaojihusisha na ukamataji na uwekaji kuzuizini watuhumiwa kinyume na sheria na kuhakikisha wanapelekwa mahakamani katika muda usiozidi saa 24 kama ilivyotakiwa kisheria," ilipendekeza.

Ripoti hiyo iliiomba Jeshi la Polisi kuhakikisha maofisa wake wanajiepusha na vitendo vya ubambikaji wa kesi na vitendo vingine vinavyokinzana na maadili.

Pia ilizitaka asasi za kiraia zishirikiane kwa karibu na Tume ya Haki za Binadamu kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu haki za binadamu kwa majaji, mahakimu na wanataaluma wa sheria ili kuwaongezea uelewa kuhusu haki za binadamu na nafasi yao katika kuzikuza na kuzilinda.

Kituo hicho pia kiliwaomba viongozi wa dini na wa jadi kutumia nafasi zao kukemea matukio ya ukiukwaji wa haki za raia, hasa haki za kuishi, uhuru wa kujieleza na haki ya kutoteswa.

Kuhusu wasichana wanaopata mimba wakiwa shuleni, LHRC iliitaka serikali kufikiria upya na kubadilisha msimamo wake wa kundi hilo, ili kulinda haki ya elimu kwao kulingana na Katiba na mikataba ya mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeiridhia.

"Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iongeze upatikanaji wa elimu kwa watoto wenye ulemavu, kwa kuhakikisha uwapo wa miundombinu inayohitajika, walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia," ilipendekeza.

## Wafunguka kuimarika diplomasia Tanzania, Kenya

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wasomi, wananchi na wafanyabiashara wamepongeza uamuzi wa viongozi wakuu wa Tanzania na Kenya, kutatua vikwazo vya uhusiano baina ya nchi hizo.

Juzi Rais Samia Suluhu Hassan, alifanya ziara ya kikazi nchini Kenya, ambayo pamoja na mambo mengine alikutana na jumuiya ya wafanyabiashara wa nchi hiyo, kuhutubia Bunge na mazungumzo maalum na Rais Uhuru Kenyatta.

Wakizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji na Mwezeshaji kutoka Taasisi ya Ujasiriamali na Uongozi wa Biashara (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema ni hatua nzuri ambayo itasaidia kufungua baadhi ya vitu na kuondoa matatizo huku suala la ushirikiano rasmi likiendelea kufanyiwa kazi.

Mchumi Mwandamizi, Prof. Samuel Wangwe, alisema kukutana kwa marais hao wa Kenya na Tanzania ni mpango mzuri hasa ikizingatiwa ni nchi jirani na Afrika Mashariki zinakwenda kwenye soko la pamoja.

Prof. Wangwe alisema hapo katikati uhusiano kati ya nchi hizo haukuwa mzuri na kwa hatua hiyo imefungua milango katika sekta mbalimbali ikiwamo biashara.

Alisema pamoja na milango kufunguliwa ni lazima utaratibu wa kununua bidhaa kutoka nchi moja kwenda nyingine ufuatwe.

Naye Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa, alisema uamuzi wa kufungua biashara na kuondoa vikwazo uliofikiwa na viongozi wa nchi hizo mbili ni mzuri kinachotakiwa kwa Watanzania kwa sasa ni kuchangamkia fursa hiyo.

**MPAKA WA HOLILI/TARAKEA**

Baadhi ya wafanyabiashara wa soko la mahindi la Himo, walisema kufunguliwa kwa mipaka kutawasababishia kujikwamua kiuchumi ikiwa ni pamoja na kujenga uhusiano bora.

"Majadiliano yaliyofanyika na viongozi hawa wawili kunaonyesha kuleta mwanga mpya kwa wafanyabiashara hasa wa mahindi, kipindi cha nyuma tulifanya kazi kwa kusuasua na baadaye tukafungiwa kabisa kusafirisha, tumepoteza mtaji lakini kwa safari ya Rais Samia tunaona matumaini makubwa," alisema Leonard Lema.

Mfanyabiashara Faustina Tairo, alisema jambo lililofanyika na viongozi wa nchi hizo mbili linaonyesha kumalizika kwa kasoro na kuboresha uhusiano.

**HOROHORO**

Wakizungumza katika mpaka wa Hororo, walisema kuzuiwa kwa biashara ya mahindi kati ya nchi hizo mbili ziliwaathiri kwa kiasi kikubwa kutokana na bei ya mahindi kushuka kutoka Sh. 60,000 kwa gunia kufika hadi 40,000.

Naye Hoza Shekwavi, alisema kuwa uamuzi huo umewapa matumaini mapya ya kuona sasa biashara za mipakani zimezingatiwa katika kuimarisha uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

***Imeandikwa na Romana Mallya, Elizabeth Zaya (DAR). Mary Mosha (MOSHI) na Lulu George (TANGA)**

# Kilichomuua Teddy Mapunda



**Na Mwandishi Wetu**

MJASIRIAMALI na mdau wa vyombo vya habari, Teddy Mapunda (pichani), amefariki dunia baada ya kuugua ghafla wakati akifuturu na marafiki zake wanahabari, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, mume wa marehemu, Nestor Mapunda, alisema Teddy alikuwa kwenye futari juzi na marafiki zake, alijisikia vibaya ghafla na kupelekwa hospitalini na ilipofika saa 5:00 usiku alifariki dunia.

"Alikuwa na tatizo la sukari, ilipanda ghafla na kusababisha matatizo mwilini ambayo yalipelekea kifo chake…tunaendelea na maandalizi atazikwa Jumatatu ijayo katika makaburi ya Kondo, Ununio, Wilaya ya Kinondoni," alisema Mapunda.

Mmoja wa marafiki wa Teddy, waliokuwa kwenye hafla hiyo, Usiah Nkhoma, alisema aliwaalika marafiki zake kwa ajili ya kufuturu pamoja kama sehemu ya kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Mwananchi Communications Limited, Bakari Machumu.

"Tulifuturu, tukafanya maongezi baada ya muda alinyanyuka akaenda kuongea na simu, baada ya muda kidogo alikuja Meneja wa Serena Hotel akatueleza kuwa mwenzenu ameanguka ghafla amepelekwa hospitalini," alisema na kuongeza:

"Tulitoka kwenda Hospitali ya Agha Khan alikopelekwa. Tulivyofika tulielezwa tumeshindwa kuokoa uhai wa mwenzenu na ameshafariki dunia. Ilikuwa masikitiko na majonzi makubwa kwetu," alisema Nkhoma.




Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya Letshego, Dk. Goodluck Meena (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Infinity Real Estate, Tumaini Mtei, wakionyesha nyaraka baada ya kusaini mkataba wa kushirikiana katika utoaji wa mikopo ya ujenzi kwa wateja wa Infinity, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA**

# DED afunguka kukataliwa na madiwani

**Na Thobias Mwanakatwe,** SONGWE

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, Hanji Godigodi, amefunguka na kueleza sababu ya madiwani wa halmashauri hiyo kuazimia kutofanya kazi naye.

Amesema hali hiyo inatokana na kukinzana kwake na madiwani hao kuhusu suala la matumizi mabaya ya fedha za serikali.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kuhusu msimamo wake baada ya madiwani katika kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Aprili 30, mwaka huu, mjini Vwawa kutangaza kususa kufanya naye kazi ambacho hakupewa nafasi kujitetea.

Mkurugenzi huyo ambaye amekuwa katika wakati mgumu kutokana na madiwani kutishiwa maisha na kutoa taarifa polisi, alitoa mfano tuhuma za ubadhirifu katika ujenzi wa Shule ya Sekondari Kisimani iliyoko Mlowo ambayo serikali ilitoa Sh. milioni 700, madiwani walihoji kwanini mkurugenzi hajasimamishwa kama ilivyafanywa kwa mweka hazina na ofisa ununuzi.

Akijibu tuhuma hizo, Godigodi alisema zipo kamati tatu zilizoundwa na mamlaka za juu ikiwamo Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ambazo zilibaini kuwa hakuhusika katika ubadhirifu huo.

Kuhusu tuhuma za ubadhirifu wa Sh. milioni 187 za kahawa kama zilivyoelezwa na madiwani, alisema ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) haikuona tatizo hilo ndiyo maana halmashauri imepata hati safi. Alisema suala lingine ni ujenzi wa uzio katika stendi ya Mlowo ambapo ilipendekezwa na madiwani zitengwe Sh. milioni 13 kwa kazi hiyo ambapo uzio huo ungetengenezwa kwa kutumia miti lakini baada ya yeye na wataalamu wake kukaa na kufanya uchambuzi, walibaini ununuzi wa miti kwa ajili ya kazi hiyo ungegharimu Sh. 1,300,000 tu na si Sh. milioni 13. Godigodi alisema katika hali ya kushangaza, licha ya jitihada zake ya kufufua magari sita ambayo yalikuwa yameegeshwa kwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, bado madiwani hao walilalamika.

Alitoa mfano wa gari aina ya Toyota V8 lililokuwa limeharibika na kuwekwa kwenye gereji ya mtu binafsi kwa zaidi ya mwaka bila kutengenezwa irudishwe halmashauri na madiwani walikuja juu kuhoji kwanini ameamuru gari hilo lirudishwe.

Godigodi alisema gari hilo lenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200 ambalo lilikuwa linatumiwa na mkurugenzi, baada ya kuharibika lilipangwa kuuzwa kwa chini ya Sh. milioni 20 tu kwa kiongozi mmoja lakini baada ya kuwasiliana na Katibu Tawala wa Mkoa wa kipindi hicho, David Kafulila, lilitengenezwa kwa Sh. milioni tisa tu na mafundi kutoka Dar es Salaam na hadi sasa linatembea kama kawaida.

Mkurugenzi huyo alisema kutokana na mambo hayo na mengine mengi, madiwani hao wamekuwa wakimwona kama adui kwao wakati yeye anafanya kazi kwa kuzingatia taratibu na sheria na walishataka kuazimia kwa zaidi ya mara mbili kutokana na misimamo yake kabla hiyo Aprili 30, walipofikia uamuzi huo.

Kuhusu maazimio ya madiwani kwenye kikao cha baraza la madiwani kwamba hawataki kufanya naye kazi, alisema atasubiri mamlaka iliyomteua ndipo ataondoka lakini si kwa shinikizo la madiwani.

# Gwajima ataka mipango muda mrefu

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe (CCM), Josephat Gwajima, amesema ili Tanzania ipige hatua katika maendeleo, serikali inapaswa kuwa na dira ya muda mrefu, kuachana na mipango ya muda mfupi.

Amesema Tanzania inapaswa kuwa na dira ya miaka 50 ambayo itawaongoza marais watakaoingia madarakani kuifuata na kuleta maendeleo. Bila kufanya hivyo, Tanzania itaendelea kudumaa. Alitoa kauli hiyo jana bungeni wakati akichangia makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2021/22.

"Nchi hii ili iendelee inapaswa kuwa na vision (dira) ya muda mrefu, ili kiongozi atakayekuja atumikie dira hiyo ambayo wananchi wameiweka na siyo dira yake," alisema Gwajima. Alisema ni vyema Tanzania ikiwa na maono ya miaka mingi vinginevyo watu wataendelea kuangamia kwa umaskini.

Alisema mataifa mengi yaliyoendelea yana dira za miaka mingi, akitoa mfano nchi ya Marekani ilikuwa na dira ya miaka 100. Gwajima alisema hata nchi ya Finland ilikuwa na dira ya miaka 40 ya maendeleo ambayo imewasaidia.

"Lakini sisi nchi yetu haina dira ya miaka mingi, ina mpango wa maendeleo ulioanzishwa na Rais mstaafu, marehemu Mkapa unaoisha 2025. Tuna ilani za uchaguzi na mipango ya muda mfupi ya miaka mitano ambayo inafanya nchi idumae," alisema Gwajima na kuongeza:

"Kwa sababu panapokuwa na mpango wa muda mrefu kwa mfano wa miaka 50 na tukaweka mkakati kuwa maendeleo yetu ni kuwa na majisafi na salama, au kila nyumba iwe na umeme au asiwapo Mtanzania atakayekaa kwenye nyumba za majani." Alisema kukiwa na dira ya miaka 50 itawabana marais watakaoingia madarakani watimize malengo yaliyowekwa.

"Lakini shida inayotusumbua sasa hivi ni kwamba tunahitaji rais mwenye maono, inamaana sisi kama nchi hatuna maono yaani rais anapoingia madarakani anatimiza maono yake namna ambavyo yeye (rais) anatafsiri maendeleo, tunajikuta tunaendelea namna kiongozi huyo anavyotafsiri maendeleo."

Gwajima alisema Tanzania inahitaji dira ya muda mrefu akitoa mfano ujenzi wa vyuo vikuu, hospitali za rufani kila wilaya ambayo itawawezesha wanafunzi kusomea masomo yanayoendana na dira hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uhusiano Tanzania na Kenya uje na fursa mpya

**RAIS** Samia Suluhu Hassan amefanya ziara ya kikazi nchini Kenya na katika hotuba yake na mwenyeji wake, Rais Uhuru Kenyatta, wametoa matumaini mapya kwa wafanyabiashara pamoja na kuimarika kwa uhusiano mzuri wa kidiplomasia kutokana na ukweli kuwa nchi hizi zinategemeana.

Kuimarika kwa uhusiano wa kidiplomasia, ni tumaini jipya kwa nchi hizo kutokana na dosari zilizojitokeza za biashara na suala la COVID-19, kiasi cha malori yenye mahindi kuzuiliwa mpakani, huku kukiwa na mchakato mrefu wa kupima corona kabla ya kuingia Kenya.

Moja ya tumaini ni suala la biashara za nchi hizo na moja ya hatua ilikuwa ni kukutana na jumuiya ya wafanyabiashara wa Kenya na Tanzania, kwa lengo la kuweka bayana msimamo wa serikali zao katika eneo hilo.

Tanzania na Kenya ndizo zina eneo kubwa la mpaka na kuna njia nne rasmi za kuingia na kutoka nchini ambazo ni mpaka wa Horohoro mkoani Tanga, Namanga mkoani Arusha, Tarakea na Holili mkoani Kilimanjaro, na kote magari na wafanyabiashara hupita kupeleka na kuingiza bidhaa nchini.

Rais Kenyatta katika hotuba yake aliagiza magari yaliyozuiwa katika mipaka mbalimbali kuingia nchini humo, ikiwa ni mwezi mmoja tangu nchi hiyo kudai kuwa mahindi ya Tanzania hayataruhusiwa kutokana na kuwa na sumu kuvu.

Katika hotuba yake Rais Samia aliwahakikishia ushirikiano na kuondoa vikwazo vyovyote vya ufanyaji biashara kati ya nchi hizo, huku masharti ya kupima COVID-19 kulegezwa ili kuimarisha ushirikiano kati ya mataifa hayo mawili ya Afrika Mashariki.

Jingine ni kupunguza au kuondoa vikwazo visivyo vya kodi vilivyopo kwenye biashara kuondolewa, lengo likiwa ni kuongeza wafanyabiashara wa nchi hizo, kukuza uchumi na kuongeza ajira.

Aidha, katika kuimarisha ushirikiano na uhusiano kati ya nchi hizo, Rais Samia alimkaribisha Rais Kenyatta kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika Desemba 9, mwaka huu.


Rais Samia akihutubia Bunge la Taifa na la Seneti jana jijini Nairobi, alisema uamuzi wa kwenda Kenya ni wa makusudi kwa kuwa ukiwa mpangaji mpya ni lazima ujitambulishe kwa majirani, na kwamba licha ya kupata mialiko mingi, lakini alianzia Kenya ili kuzungumza na kuimarisha uhusiano wa kipekee uliopo kati ya nchi hizi, ambao ni wa damu na haitengenishiwi na mipaka iliyopo, kwa kuwa makabila yanaingiliana licha ya kupakana na nchi nane.

Watanzania wanaamini kuwa kuboreshwa kwa uhusiano wa nchi hizi zinazotegemeana kwa kiasi kikubwa, utaimarisha uhusiano na ujirani mwema kwa manufaa ya nchi zote kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo na sasa ni wajibu wao kutambua fursa na kuzitumia vyema.

Kuimarika kwa uhusiano wa nchi zinazotegemeana ni manufaa kwa wananchi wake kwa kuwa sasa milango ya ushirikiano itaimarika kwa kufanya biashara ambazo zinakwenda kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi zote.

Ni muhimu sana kwa Watanzania kutumia vyema fursa hiyo kwa kufanya biashara na kuwekeza Kenya hasa kwa wakati huu ambao Rais Kenyatta ametangaza kuondolewa kwa vikwazo vilivyokwamisha biashara kati ya nchi hizo. Fursa za biashara na uwekezaji kwa nchi hizo ni muhimu sana kwa kuwa nchi zinategemeana, mathalani kwa sasa ruhusa ya kusafirisha mahindi kwenda nchini humo, ambako ilikuwa ndiyo soko kuu la bidhaa hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kufanikisha vita dhidi ya malaria, inahitajika elimu ya chandarua

Na Sabato Kasika

**SIKU** zilizopita Tanzania iliungana na nchi nyingine duniani, kuadhimisha Siku ya Malaria Duniani, ambayo ilikuwa na kaulimbiu isemayo: 'Tumia chandarua kilichotiwa dawa kitatukinga na malaria.'

Siku hiyo huadhimishwa Aprili 25 ya kila mwaka, kwa ajili ya kutafakari vita dhidi ya ugonjwa na kuweka mikakati zaidi ya kukabiliana nao ikiwamo matumizi ya vyandarua chenye ambayo yamekuwa yakihimizwa.

Pamoja na kwamba jamii imekuwa ikihimizwa kutumia vyandarua vyenye dawa, wapo baadhi ya watu hawavitumii, kwa madai yasiyo na msingi, kwamba dawa za kuua mbu zilizowekwa kwenye vyandarua hivyo, vinapunguza nguvu za kiume.

Kutokana na imani hiyo, wengine huchukua vyandarua hivvyo na kufanikia vifaranga vya kuku, kuzungushia bustani zao za mbonga na kuacha matumizi sahihi ambayo yamekusudiwa ili kuwaepusha na ugonjwa huo.

Ili kukabiliana na ugonjwa huo, inaelezwa ni muhimu kuimarisha usafi wa mazingira, kuondoa mazalia ya mbu, pia kufuata matumizi sahihi ya vyandarua vilivyoweka dawa za kuua mbu.

Lakini kila mtu anatakiwa kunyunyiza dawa sehemu ambazo kuna mazalia ya mbu ikiwa ni miongoni mwa mikakati ya kuhakikisha malaria inakoma kwenye jamii na kuwa na afya salama.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Kanda ya Afrika, Mwakilishi Mkazi wa shirika hilo Zanzibar Dk. Ghirmany Andermaechal, anasema malaria inaendelea kuwasumbua wananchi wengi katika bara hili na kusababisha vifo vingi.

Ili kusaidia kupunguza au kutokomeza ugonjwa huo, ninadhani kuna haja ya kuwapo elimu ya kutosha kwa watu ambao hawataki kutumia vyandarua, kutokana na imani zinazowapotosha.

Ni utafiti gani ambao waliufanya hadi wakagundua kuwa dawa zilizowekwa kwenye vyandarua zinapunguza nguvu za kiume? Watu wa aina hii wakielimishwa wanaweza kuachana na imani hiyo.

Imani hiyo inaweza kuwa inachangia kuendelea kuwapo kwa ugonjwa huo ndani ya jamii, kwa kuwa wahusika wanaweza kuvuta watu wengi zaidi wakaamini hicho wanachodai bila kufanya utafiti.

Binafsi ninaamini, hadi kitaalamu na kwa idhini ya mamlaka kuu ya afya duniani WHO, ikaruhusiwa matumizi ya vyandarua hivyo, imeshajiridhisha kuwa havina madhara kwa watumiaji, kuwapo kwa watu wanaoamini kuwa vinapunguza nguvu za kiume, basi elimu inahitajika.

Jamii ielimishwe umuhimu wa matumizi ya vyandarua hivyo kuwa pamoja na kwamba vina dawa, haipunguzi nguvu za kiume, bali inaua mbu na hivyo kuwasaidia kujinga na malaria.

Kaulimbiu ya mwaka huu isemayo: 'Tumia chandarua kilichotiwa dawa kitatukinga na malaria.' ni elimu tosha ambayo kwa namna moja au nyingine, inaweza kuwa na mchango mkubwa katika vita dhidi ya malaria.

Pia si vibaya wataalamu wa afya kuzunguka maeneo mbalimbali nchini kujionea hali halisi ya matumizi ya vyandarua, ili wale ambao wanavitumia isivyo kwa kudhani vina madhara, basi waelimishwe.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalowahudumia Watoto (UNICEF), linaweka wazi kuwa vyandarua maalum vilivyotengenezwa na kunyunyiziwa dawa ya kuua mbu, hivi sasa vinaokoa maisha ya wanavijiji wengi hapa nchini.

UNICEF inakaririwa katika maadhimisho ya mwaka huu ikisema kuwa, malaria umekua ukiua watoto chini ya umri wa miaka mitano, wazee na akina mama wajawazito, na kwamba vifo hivyo vimeanza kupungua.

Ili kukabiliana na maambukizo, ninaamini elimu kuhusu matumizi ya vyandarua ni ya muhimu ili kuondoa imani potofu ambayo kwa namna moja au nyingine, inachangia kuendelea kuwapo kwa ugonjwa huo nchini.

HABARI KITAIFA

# Waziri aonya wapiga majungu kazini

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, amewaonya watumishi na viongozi wa taasisi za umma kuacha majungu mahala pa kazi jambo ambalo limekuwa likirudisha nyuma maendeleo.

Badala yake, kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kuleta tija na ufanisi katika utumishi wa umma.

Mchengerwa aliyasema hayo juzi wakati wa ziara yake ya kikazi ya kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma na kukagua utekelezaji wa miradi ya kunusuru kaya maskini inayotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wilayani Magu.

Alisisitiza kuwa watumishi na viongozi wasiowajibika hawana nafasi katika Serikali ya Awamu ya Sita ambayo imedhamiria kutoa huduma bora kwa wananchi na kuongeza kuwa atahakikisha utumishi wa umma unakuwa na rasilimali watu yenye tija.

Waziri alisema utumishi wa umma ndiyo injini ya nchi, hivyo viongozi na watumishi wa umma hawana budi kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mchengerwa alisema kuna baadhi ya viongozi na watumishi wenye nyadhifa wamekuwa wakitumia nafasi zao kukandamiza watumishi walio chini yao kwa kusikiliza majungu na fitina.

"Tuache kutumia nyadhifa tulizo nazo vibaya, hivyo tufanye kazi na kama kuna mtumishi ambaye amekuwa akitekeleza majukumu yake kikamilifu apewe ushirikiano na aendelezwe ili kutoa mchango mkubwa kwa taifa badala ya kujengewa uadui," alisema.

Aidha, aliwataka watumishi wa umma kuwa na utamaduni wa kujiendeleza ili kufika mbali.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kulia), akibadilishana nyaraka na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Bernard Konga (wa pili kushoto), baada ya kusaini makubaliano ya kurahisisha upatikanaji wa bima ya afya kwa wakulima wa mazao ya kimkakati, mbele ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania, Dk. Benson Ndiege (wa tatu kushoto), jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa (wa pili kulia), Mwanasheria wa Benki ya CRDB, Pascal Mihayo (kulia), Mwanasheria wa NHIF, Benjamin Mwalugaja na Mkurugenzi wa Wanachama wa NHIF, Christopher Mapunda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CRDB, NHIF zajitosa kusaidia wakulima

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI ya CRDB imetia saini mkataba wa makubaliano na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wenye lengo la kurahisisha upatikanaji wa bima ya afya kwa wakulima nchini.

Akizungumza wakati wa kutia saini mkataba huo, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema wameshirikiana ili kuwasaidia wakulima kupata bima ya afya kwa mkopo.

"Katika makubaliano hayo, CRDB itakuwa ikisaidia kulipa gharama za bima ya afya (premium) na wakulima kulipa mwisho wa msimu baada ya kuuza mazao lengo kuhakikisha tunawakomboa na wao kwenye upande wa afya ili waendelee na shughuli zao bila kukwama," alisema Nsekela.

"Ushirikiano huu wa Afya Premium Loan ni huduma ambayo itatolewa kwa wakulima ambao wako katika vyama vya ushirika na itawanufaisha pia wategemezi wao, kwa maana ya mke au mume na watoto na mkopo utatolewa kulingana na kiwango cha gharama za malipo ya bima ya afya husika," aliongeza.

Nsekela alisema wamefanya hivyo ili kuhamasisha wakulima kukata bima kwa familia zao.

"Lengo letu ni kusaidia jitihada za serikali kuboresha afya za Watanzania kwa kuhakikisha Watanzania wote wanapata bima ya afya kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza.

"Ukiboresha afya ya mkulima, umeboresha afya ya Tanzania na ni imani yangu kuwa utaratibu huu wa bima ya afya utakuwa suluhisho kubwa ya kila mkulima kuipatia kaya yake uhakika wa matibabu wakati wowote," alisema Nsekela.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema mfuko huo umejipanga kuhakikisha unawahudumia kikamilifu wakulima ili wawe na uhakika wa shughuli zao katika kipindi chote cha mwaka.

"Lengo kubwa la mpango huu ni kuwawezesha wakulima wawe na uhakika wa afya zao kwa maana ya kupata huduma za matibabu wakati wowote wanapozihitaji na kwa upande wa mfuko tumeboresha zaidi huduma zetu ili mwanachama wetu asipate usumbufu wa aina yoyote," alisema Konga.

Alisema endapo wakulima wataitumia fursa hiyo vizuri, itawapa ufanisi katika uzalishaji mali kwa kuwa wakati wote watakuwa na amani na mapato yao yatatumika kwa maendeleo na sio kulipia huduma za matibabu.

# TAKUKURU Iringa yaokoa milioni. 158/-

**Na Francis Godwin,** IRINGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa imeokoa shilingi 158,066,810, ambazo zinadaiwa kuchepushwa.

Akitoa taarifa ya utendaji kazi ya miezi mitatu, mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Iringa, Domina Mukama, alisema fedha hizo zimeokolewa kati ya Januari 2021 na Machi 2021 kupitia uchunguzi uliofanywa katika ofisi zote za mkoa wa Iringa.

Alisema uchunguzi huo pia unahusisha fedha ambazo zilikuwa zichepushwe au kufanyiwa ubadhirifu.

Aidha, alisema kwa kipindi hicho taasisi hiyo imefanikiwa kufanya uchambuzi wa mfumo unaohusu utoaji vibali vya ujenzi katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Kilolo, na Mji Mafinga zoezi ambalo lilifanyika baada ya kupokea malalamiko kuhusu ujenzi holela katika halmashauri husika.

Kuhusu ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo, alisema taasisi yake katika kuzingatia usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo imefanya ukaguzi wa miradi mitano ya maendeleo yenye thamani ya shilingi 1,352,390,557.50 kwa kukagua mradi wa ukarabati wa barabara ya Izazi -Mboliboli -Pawaga yenye urefu wa kilomita 36 yenye thamani ya shilingi 325,436,325.

Pia ufuatiliaji wa utekelezaji wa mfuko wa maendeleo ya jamii (TASSAF III) katika Manispaa ya Iringa wenye thamani ya shilingi 115,286,442.50, pia ufuatiliaji wa mfuko wa TASSAF III katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo wenye thamani ya shilingi 201,454.140 pamoja na ukaguzi wa mradi wa matengenezo ya kawaida, uboreshaji wa maeneo korofi, ujenzi wa karavati na ujenzi wa mifereji kiwano cha mawe wenye thamani ya shilingi 250,000,000 katika barabara za mji wa Mafinga.

Kadhalika, Takukuru imekagua mradi wa ujenzi wa kilomita moja ya barabara ya kiwango cha lami katika barabara ya kwamkoa-Mbagala, Mgaya II na Kanani na ujenzi wa mtaro na karavati wenye thamani ya shilingi 460,213,650 katika Halmashauri ya Mji Mafinga, Wilaya ya Mufindi.

# Walilia mishahara miezi minne sasa

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAFANYAKAZI 89 wa kiwanda cha kutengeneza dawa za kuulia viluilui vya mbu kilichoko Kibaha mkoani Pwani, wamelalamikia kufanya kazi bila mishahara kwa miezi minne sasa.

Wakizungumza na waandishi wa habari juzi, wafanyakazi hao walisema wamekuwa wakiishi maisha magumu kutokana na kukosa haki zao kwa muda mrefu huku kukiwa hakuna taarifa kutoka kwa viongozi wao namna watakavyopata malipo yao.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi hao, Ofisa Ubora na Udhibiti wa Kiwanda hicho, Dk. Nicholas Banzi, alisema pamoja na deni la mishahara pia bima za afya hazilipwi kwa wakati.

Alisema katika kufuatilia mishahara yao wameambiwa kuwa shirika halina fedha kwa sasa jambo ambalo limeendelea kuwapa wakati mgumu huku wakiendelea na kazi ya uzalishaji wa dawa hizo.

"Hi si mara ya kwanza kuwa na madai kama haya. Tumekuwa tukikosa mishahara mara kwa mara na wakati huu imefika miezi minne sasa hatujalipwa. Tunazidi kutaabika na familia zetu tunaomba serikali iingilie kati," alisema.

Naye John Tusiwe alisema kilipoanzishwa kiwanda hicho walikuwa wakilipwa vizuri, lakini ilipofika 2017 walitolewa kwenye utaratibu wa malipo ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC).

Tusiwe alisema jambo la kushangaza ni kwa viongozi wa ngazi za juu wanaendelea kupata mishahara kama kawaida huku wafanyakazi wao wakitaabika.

Akizungumzia kuhusu malalamiko hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Mhandisi Martine Ntemo, alikiri kupata taarifa za wafanyakazi hao.

Ntemo alisema tayari Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ametembelea katika kiwanda hicho na kufanya kikao na wafanyakazi kujadiliana namna ya kutatua tatizo hilo.

Mkuu huyo wa wilaya alisema hali ya kiwanda hicho kwasasa hairidhishi kwani wizi wa baadhi ya vifaa umeanza kutokea kutokana na walinzi kukosa mishahara tangu mwaka 2020 na hivyo kushindwa kuimarisha ulinzi katika kiwanda hicho.

"Waziri amekuja na fedha kiasi kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi lakini fedha hiyo haitoshelezi. Hata mishahara ijayo haina uhakika," alisema.

Ntemo alisema katika kikao hicho, iliwekwa mikakati ya muda mfupi ambayo ililekezwa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kuona namna ya kupata mishahara huku shughuli za kiwanda zikiendelea.

Kuhusu mikakati ya baadaye, alisema walijadili kuona namna ya kuanza kutengeneza dawa za kilimo na kufanya utafiti wa soko kabla ya kuanza.

Alisema waziri huyo alitoa wiki moja kwa timu ya taifa ya mashauriano kufanyia kazi mikakati hiyo na kutoa majibu ikiwamo mikataba ya wafanyakazi.




Meneja Mwandamizi wa Bima wa Benki ya NMB, Catherine Joshua (katikati), akibofya kitufe kumpigia simu mmoja wa washindi wakati wa droo ya saba ya shindano la 'Bonge la Mpango' iliyofanyika katika NMB Tawi la Mbezi Louis, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Ofisa Mkaguzi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga na Ofisa Huduma kwa wateja, Neema Kazaviyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NHC kujenga nyumba 1,000 Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa nchini (NHC), liko mbioni kukamilisha ujenzi wa nyumba 400 kati ya 1,000 mkoani Dodoma kwa ajili ya Watanzania na watumishi wanaohamia hapa.

Pia shirika hilo limefanya maboresho kadhaa kwenye nyumba hizo ikiwamo kushusha gharama za mauzo ambapo kwa sasa ni kati ya Sh. milioni 59 hadi 99. Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulidi Banyani, alibainisha hayo jana jijini hapa kwenye ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa nyumba hizo katika maeneo ya Chamwino na Iyumbu.

Alisema hatua hiyo inalenga kusaidia upatikanaji wa makazi hasa baada ya uamuzi wa serikali kuhamishia shughuli za serikali jijini Dodoma na kwamba nyumba hizo zinajengwa kwa awamu tatu.

"Ili kuwezesha ujenzi wa nyumba nyingi za makazi jijini Dodoma, serikali imelipatia shirika mkopo nafuu wa Sh. bilioni 20 zitakazotumika kama mtaji wa kujenga nyumba 1,000 na zitauzwa au kupangishwa kwa wananchi. Kwa sasa shirika liko kwenye awamu ya kwanza ya ujenzi kwa nyumba 400 zitakazogharimu Sh. bilioni 21.4," alisema.

Alibainisha kuwa awamu ya pili itakuwa ujenzi wa nyumba 325 na majengo sita ya huduma zitajengwa Chamwino na Mahoma na awamu ya tatu ni ujenzi wa nyumba 275, ndani ya miaka miwili hadi mitatu zitakuwa zimejengwa.

"Tumekadiria kutumia Sh. bilioni 71 kwa ujenzi wa nyumba zote 1,000. Bei ya nyumba zinazojengwa itaanzia Sh. milioni 59 hadi 99 ikitegemeana na ukubwa wa nyumba na kiwanja husika," alisema.

Alisema nyumba 100 kati ya 400 zilizojengwa kwa awamu ya kwanza ambazo ziko Chamwino zitapangishwa huku nyumba 300 zitauzwa kwa gharama nafuu ikilinganishwa na gharama za nyumba zilizojengwa miaka minne iliyopita.

"Nyumba za awamu ya kwanza ziliuzwa kwa Sh. 861,400 kwa mita moja ya mraba na nyumba za sasa zinauzwa kwa Sh. 797,730 kwa mita moja ya mraba. Gharama zimepungua kwa Sh. 63,000 kwa mita moja ya mraba," alisema.

Hata hivyo, alisema nyumba za sasa ni kubwa na ziko kwenye viwanja vikubwa vyenye ukubwa unaoanzia mita za mraba 600 na kuendelea wakati nyumba za awali zilikuwa na ukubwa wa mita za mraba 300.

Alitoa wito kwa Watanzania kuchangamkia nyumba hizo na kwamba zimejengwa kwa viwango na ubora wa hali ya juu.

# TBS yasajili majengo biashara ya chakula

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limefanya usajili wa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi mkoani Pwani pamoja na ukaguzi wa kushtukiza madukani.

Katika ukaguzi huo, maofisa wa TBS wamechukua sampuli za bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi ili kuzipima kwenye maabara za shirika kujiridhisha kama zinakidhii ubora.

Lengo la TBS kusajili majengo ya chakula na vipodozi uliofanyika mkoani Pwani kuanzia Aprili 7 hadi 21, mwaka huu, ni kuwawezesha wafanyabiashara kufanya shughuli kwa kufuata matakwa ya sheria na kuzingatia kanuni bora za afya ili kulinda afya za watumiaji.

Miongoni mwa majengo yaliyofanyiwa ukaguzi na usajili ni pamoja na migahawa, baa, mashine za kusaga, majengo ya kuuza vyakula na maduka ya vipodozi. Akizungumza na waandishi wa habari juzi mkoani Pwani, Ofisa Masoko wa TBS, Rhoda Mayugu, alisema walifanya kazi hiyo katika maeneo ya Kibaha Mjini, Kibaha kwa Mathias, Kongowe, Mlandizi, Chalinze na Bagamoyo.

Kuhusu ukaguzi wa kushtukiza, alisema walinunua sampuli za vifaa vya ujenzi, zikiwamo nondo, mabati, sementi na bidhaa za vyakula kwa ajili ya kwenda kujiridhisha kama zinakidhi ubora.

Mayugu alisema mwitikio wa wafanyabiashara kusajili majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi ni mkubwa hasa kutokana na elimu ambayo wamekuwa wakiipata kwamba majukumu hayo kwa sasa yapo chini ya TBS, badala ya iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA).

Kwa Mujibu wa Mayugu, usajili wa majengo ya vyakula na vipodozi una faida nyingi, ikiwa ni pamoja na kuwezesha wafanyabiashara kutambulika kuwa wana vibali vya kusajiliwa majengo ya bidhaa za chakula na vipodozi.

Kuhusu mkakati wa shirika hilo kufikia wafanyabiashara wote, Mayugu alisema usajili huo ni endelevu ili kuhakikisha majengo yote ya bidhaa za chakula na vipodozi yanasajiliwa kwa kuwa hilo ni takwa la kisheria. Mayugu aliwataka wafanyabiashara pale wanapoanza kufuatilia leseni kwa ajili ya kuanza kufanya biashara wahakikishe wanajisajili TBS kwa kuwa utaratibu ni rahisi na rafiki na kwamba wanaweza kufanya hivyo kwa njia ya mtandao, hivyo hakuna sababu ya kufika kwenye ofisi za shirika hilo.

HABARI KITAIFA

## Mifugo sasa kupimwa uzito kabla ya kuuzwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI inaweka utaratibu wa kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito badala ya kukisia kama inavyofanyika sasa kwenye minada na maeneo mengine.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba wakati akifungua mafunzo ya kwa wafanyabiashara na wajasiriamali wa mkoa huo yaliyoandaliwa na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuwawezesha kujua umuhimu wa vipimo sahihi.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, Mumba alisema wanatakiwa kuhakikisha minzani wanayotumia wale wanunuzi iko sawa.

"Kwa hiyo nazishauri mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kwenye maeneo yao kuna masoko mbalimbali yakiwamo magulio na baadhi ya minada, haina vipimo sahihi au haitumii mizani, kwa hiyo tunapoendelea Serikali inaweka utaratibu kuhakikisha mifugo yote inauzwa kwa kupimwa uzito badala ya kukisia," alifafanua Mumba.

Alisema kwa kadri wananchi watakavyozingatia suala la vipimo, manufaa yake yataonekana kwa wadau wote, anayezalisha na yule anayekwenda kutumia hiyo bidhaa, kwani atakuwa na uhakika kwamba thamani ya fedha yake inalingana na kitu kile ambacho amepewa.

"Hicho ndicho kikubwa zaidi kwani pande zote zinafaidika na matumizi sahihi ya vipimo," alisema Mumba.

Alisema semina hiyo itawezesha wafanyabiashara na wenye viwanda kuweza kuelewa kwa kina suala la uzingatiaji wa vipimo sahihi.

Kwa mujibu wa Mumba, kupitia kampeni mbalimbali, Serikali imekuwa ikiendesha kaguzi ili kuhakikisha wananchi na wadau wote wanazingatia suala zima la vipimo kutokana na unyeti wake katika maendeleo ya nchi yetu.

Aliongeza kwamba wamekuwa wakipokea malalamiko kadhaa kuhusiana na matumizi batili ya vipimo kwenye mkoa huo na kupitia WMA, wameendelea kushirikiana kuhakikisha wadau wote wanaendelea kutumia vipimo sahihi.

Alifafanua zaidi kwamba Dodoma peke yake kuna viwanda zaidi ya 3,000, vikiwamo vya kusindika alizeti, unga, viwanda vya mvinyo, hivyo suala la kuzingatia vipimo ni muhimu sana kuanzia shambani wakulima wanapokuwa wanapouza mazao.

Kwa upande wake Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kahwa, alisema WMA jukumu lake kuu ni kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo.

"Kwa hiyo tuna kazi ya kuhakiki vipimo na kuhakikisha vinatumika kwa usahihi," alisema na kuongeza;

"Tuna jukumu la kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu zinafungashwa kwa usahihi, kwa sababu ili uweze kupenya kwenye soko la kimataifa ni lazima ufungashaji wa bidhaa zako uzingatie miongozo yote ya Shirika la Vipimo Duniani."

Alisema WMA ni mwanachama hai wa Shirika la Vipimo Duniani, hivyo wao wanatakiwa kutoa miongozo hiyo kwa wazalishaji wa ndani ili waweze kushindana kimataifa na kitaifa.

Aliongeza kwamba ili kuelekea Tanzania ya Viwanda , lazima vipimo sahihi vizingatiwe na kwamba wanafanya semina za aina hiyo nchini kote ili kuwafikia wafungashaji na wazalishaji wadogo wadogo ili waweze kukua, wawe wazalishaji na wafungashaji wa kati na mwisho wa siku wawe wa kimataifa.

"Kwa hiyo tunatumia semina hizi kwa ajili ya kuwaelimisha wafungashaji na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali nchini na sasa tupo Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine zimekwisha fanyika semina na mafunzo kama haya kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda Tanzania," alisema Kahwa.

Naye Kaimu Meneja wa WMA Mkoa wa Dodoma, Karim Zuberi, alisema semina hiyo ni kwa ajili ya kuelimisha matumizi sahihi ya vipimo na ufungaji kwa wafanyabiashara na wajasiriamali mbalimbali wenye viwanda na wengineo.

# Wanawake 4,000,000 wapata elimu kutambua haki za ajira

**Na Elizabeth Zaya**

WANAWAKE milioni nne wamepata elimu ya kutambua haki na sheria za ajira nchini.

Wanawake hao wamepata fursa ya kupata elimu hiyo kutoka katika Kituo cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), kupitia mradi wake wa uwezeshaji wa kisheria na haki za ajira unaofadhiliwa na Legal service Facility ( LSF).

Mkurugenzi Mtendaji wa WLAC, Theodosia Muhulo, alisema mradi huo ni wa kuboresha mazingira ya kazi na kupunguza visababishi vya ukiukwaji wa haki na sheria za ajira nchini ukilenga wanawake, vijana na wanaoishi na ulemavu katika sekta rasmi na isiyo rasmi, wafanyakazi wa viwandani na majumbani.

Muhulo alisema mbali na kuboresha mazingira ya kazi, pia ulilenga kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa haki kwa wakati katika mifumo ya utoaji haki hizo na kuboresha uwezo wa wanawake na vijana katika kudai haki zao. "Katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa mradi huu, tumefikia wanawake milioni nne waliopata elimu juu ya haki na sheria za ajira kupitia matangazo, machapisho, jumbe za[EZI] kuelimisha, mitandao ya kijamii na uelimishaji kupitia msaada wa sheria unaotembea," alisema Muhulo.

"Pia,WLAC imetoa msaada wa sheria kwa wafanyakazi 672 na kati ya hao 432 wamepewa msaada wa kisheria katika mashauri yao. Tumewafikia wadau 203 wa vyama vya wafanyakazi katika mafunzo mbalimbali katika kuwaelimisha masuala muhimu yanayohusu sheria na usawa wa jinsia katika maeneo ya kazi."

Alisema elimu hiyo iliyotolewa pia kwa waajiri, imewasaidia wengi wao kuelimika na kuanza kufuata sheria na taratibu za ajira ikiwamo kuwapa wafanyakazi mikataba ya ajira, likizo na kuzingatia makato yaliyoainishwa kisheria.

"Vyama vya kutetea haki za wafanyakazi baada ya kupata mafunzo haya, navyo vimeanza kuzingatia majukumu yao na hata kuwaelimisha watumishi wao kusimamia masuala yanayohusu ukiukwaji wa haki hizo," alisema Muhulo.

Alitoa wito kwa wanawake na wafanyakazi katika sekta mbalimbali, kuwa wajasiri na kupigania haki zao pale zinapokiukwa.



Wateja wa Benki ya Stanbic Tawi la Kariakoo jijini Dar es Salaam wakimsikiliza Meneja wa tawi hilo, Said Salehe (hayupo pichani), wakati wa futari iliyoandaliwa na kampuni ya Silent Ocean kwa ajili ya wateja wao, ambapo benki hiyo iliahidi kuongeza ushirikiano na Kampuni ya Silent Ocean ili kuwawezesha wafanyabiashara nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Siri ya kufikia maendeleo ya TEHAMA hii

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameelezea namna ya kufikia maendeleo ya Teknolojia Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili kukuza uchumi wa nchi.

Amesema serikali ipo tayari kuhakikisha kuwa miundombinu ya TEHAMA inakuwa bora ili kufikia malengo hayo.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa Taasisi ya Watendaji Wakuu Dar es Salaam (CEOrt) uliofanyika juzi Dar es Salaam na kukutanisha wanachama wake.

Mkutano huo ulijadili namna ya kuondoa vikwazo kwenye sekta hiyo na kuunganisha teknolojia ya kisasa na kuchochea maendeleo nchini.

Dk. Ndugulile alisema kunahitajika uwekezaji zaidi katika sekta hiyo ikiwamo kutoa mafunzo ili kuongeza ushindani.

"Tunafahamu umuhimu wa sekta binafsi nchini, ndio maana tutaendelea kushirikiana nayo pamoja na taasisi hii katika utekelezaji na ukuaji wa teknolojia ikiwamo kuunganishwa wananchi kwenye matumizi ya uchumi wa kidigitali," alisema Dk. Ndugulile.

Kwenye mkutano huo waziri alipokea changamoto za sekta hiyo kutoka taasisi ikiwamo mbinu za kukabiliana nazo na kwamba marekebisho ya sera ambayo yamefanyika hivi karibuni yamesaidia sekta ya mawasiliano kuwa kati ya sekta huru nchini.

Kati ya changamoto hizo ni pamoja na ushindani wa kibiashara ambao ulitokea hivi karibuni ikiwamo kupanda viwango vya huduma za simu, ikizingatiwa matumizi ya mtandao yaliongezeka kipindi cha corona.

Mkurugenzi wa Benki na Mwenyekiti wa CEOrt, Sanja Rughani aliishukuru serikali kwa kuendelea kufanya kazi pamoja hususan kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano na kusaidia kukuza viwanda.

"Ninaamini serikali itajikita kwenye TEHAMA, nchini na leo tumekutana kujua namna ya kutimiza malengo yetu, tunahitaji kufanya kazi bega kwa bega na serikali," alisema Rughani.

# Eneo uwekezaji kutokugawanywa

WIZARA ya Kilimo imesema haitaligawa eneo la uwekezaji lililotengwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) mkoani Mtwara kwa matumizi mengine kwa kuwa bado linahitajika kwa shughuli za uwekezaji.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Anastazia Wambura, aliyetaka kujua kuhusu eneo hilo ambalo limeendelezwa kwa kiasi kidogo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Bashe alisema serikali itaendelea kulihifadhi eneo hilo la uwekezaji mkoani Mtwara kwa ajili ya kuliendeleza kwa awamu kadri mahitaji yanavyojitokeza huku akitoa wito kama kuna wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye eneo hilo wanakaribishwa.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alitaka kuja ni kwa kiasi gani eneo hilo la uwekezaji la EPZ mkoani Mtwara limetumika kwa shughuli iliyokusudiwa.

Naibu Waziri Bashe akijibu swali hilo, alisema mradi wa ujenzi wa Bandari Huru ya Mtwara unahusu ujenzi wa sehemu maalum ya bandari yenye gati na sehemu ya ugavi kwa ajili ya kuhudumia sekta za mafuta na gesi.

Alisema madhumuni ya kuanzishwa kwa eneo la uwekezaji katika eneo la Bandari Huru ya Mtwara ilitokana na hitaji la kampuni zinazotoa huduma kwa kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji wa gesi na mafuta katika mwambao mwa Pwani ya Tanzania, Kenya na Msumbiji ambayo yalikuwa yanahitaji kuwa na kituo cha ugavi karibu na Bandari ya Mtwara.

Pia alisema eneo la mradi wa uwekezaji lenye ukubwa wa jumla ya hekta 110 katika Bandari Huru ya Mtwara linaendelezwa kwa awamu.

"Katika awamu ya kwanza, eneo la ukubwa wa hekta 10 limeendelezwa kwa asilimia 100 kama ilivyopangwa, shughuli za utekelezaji wa mradi huo zimehusisha ujenzi wa miundombinu wezeshi ya ndani na nje ikiwamo barabara kwa kiwango cha lami, umeme na mfumo wa usambazaji wa majisafi," alisema Bashe.

Naibu Waziri huyo alisema kutokana na uendelezaji wa miundombinu katika eneo hilo kukamilika kwa asilimia 100, kwa sasa shughuli za uwekezaji katika eneo hilo zinaendelea vema na kampuni tatu zinafanya shughuli za uwekezaji.

# Mbunge alia msongamano wanafunzi

MBUNGE wa Mbagala (CCM), Jafari Chaurembo, ameiomba serikali kujenga shule mpya za kutosha katika jimbo hilo kutokana na kukabiliwa na idadi kubwa ya wanafunzi wa msingi na sekondari.

Amesema hatua hiyo imechangia kuwapo msongamano wa wanafunzi kwenye baadhi ya shule.

Akiuliza maswali bungeni jana, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuipa fedha Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ili kujenga shule mpya za kutosha kutokana na jimbo hilo.

Pia Chaurembo alisema hiyo ni kutokana na kuwa sera ya serikali ni kuwa na shule za sekondari katika kila kata nchini.

"Serikali ina mipango gani wa kujenga sekondari hizo katika kata zake za Mbagala, Kilungule na Kibonde Maji? alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema ili kuboresha miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, katika mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 serikali iliipatia Sh. milioni 724.

Silinde alisema fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya msingi ya Marten Lumbanga na Shule ya Msingi Dovya.

"Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/21 halmashauri hiyo kupitia mapato yake ya ndani, imejenga jengo la ghorofa moja kwa ajili ya kidato cha tano na sita katika Shule ya Sekondari Mbagala kwa gharama ya Sh. bilioni 1.056," alisema.

Pia alisema alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imeitengea Temeke Sh. bilioni 1.74 ambapo Sh. bilioni 1.53 zitaelekezwa katika jimbo hilo kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya katika Kata ya Chamazi.



Habari na Augusta Njoji

"Katika mwaka wa fedha 2017/18 serikali ilikamilisha maboma 10 ya madarasa ya shule za msingi katika Halmashauri ya Temeke kwa gharama ya Sh. milioni 137.5," alisema.

"Kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi 2019/20 serikali imejenga madarasa mapya 25 ya shule za msingi katika halmashauri hiyo kwa gharama ya Sh. milioni 500," alisema.

Silinde alisema katika mwaka wa fedha 2020/21 Temeke kupitia mapato yake ya ndani, imejenga vyumba 76 vya madarasa ya shule za sekondari kwa gharama ya Sh. bilioni 1.72.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga Sh. milioni 220 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 11 vya madarasa ya shule za sekondari katika halmashauri hiyo na Sh. milioni 209 zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya shule za sekondari," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali itajenga shule za sekondari 1,000 nchi nzima katika kata ambazo hazina shule hizo ikiwamo za jimbo hilo.



Mbunge wa Namtumbo, Vita Kawawa (kulia), akijadiliana jambo na Mbunge wa Mvumi, Livingstone Lusinde (kushoto), bungeni jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# JMT, SMZ kuangalia bei ya umeme

IMEELEZWA kuwa serikali ya Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimeendelea kushughulikia suala la bei ya kuuza na kununua umeme baina ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ili kuupatia ufumbuzi mgogoro huo.

Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato alibainisha hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Jang'ombe (CCM), Ali Omari King.

Mbunge huyo, katika swali lake, alitaka kujua ni lini serikali itatua mgogoro wa bei ya umeme unaotumika na Watanzania waishio Zanzibar ili kuweka usawa kwa Watanzania wote.

Byabato alisema katika kipindi cha mwaka 2020/21 timu ya wataalamu wa taasisi husika zilikutana katika vikao mbalimbali na kufanya uchambuzi wa kina wa vigezo vilivyotumika katika kupanga bei umeme kwa wateja wakubwa wa kununua umeme ikiwamo ZECO.

Alisema kutokana na uchambuzi huo, inapendekezwa kuwa vigezo hivyo vipitiwe upya ili kuleta unafuu kwa wateja wa aina hiyo, ikiwamo ZECO.

Byabato alisema mapendekezo hayo yaliwasilishwa katika kamati ya wizara zinazoshughulikia masuala ya muungano ili kufanya kazi na kupata ufumbuzi wa suala hilo.

ama
ALHAMISI MEI 6, 2021
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Mkoa Manyara unavyong'ara katika operesheni chanjo wajawazito, watoto**



Ukurasa 13

**Unajua msamaha unakuepusha na mlolongo wa maradhi mwilini?**

# Hospitali rufani zote kupata huduma dharura na mitungi mikubwa ya gesi

## ■Bomba hadi wodini, zahanati kunufaika

**Na Yasmine Protace**

HUDUMA za dharura katika afya, inatajwa kuwa moja ya nyenzo muhimu za mafanikio ya uokoaji maisha ya mgonjwa, anapofika hospitalini akiwa na hali mbaya.

Huduma za dharura zinasaidia hata mgonjwa wa dharura hakai foleni kwa ajili ya kumsubiri daktari, ili apate matibabu. Utaratibu wake, mgonjwa anapatiwa huduma mara moja anapofikishwa hospitali.

Sehemu kubwa za tiba, mfano katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, zina kitengo mahsusi cha kuhudumia wagonjwa wa dharura.

Kinachoendelea sasa nchini, ni kwamba sehemu zote kubwa za tiba za kiserikali, zinaazimiwa kupatiwa huduma hizo za dharura.

Hadi sasa serikali inaendelea kutimiza hilo, katika hospitali saba za rufani za mikoa, zimeshakuwa na huduma ya dharura, ili kuwanufaisha wagonjwa wa dharura.

Ni hatua inayoendana na kusimikwa mitambo ya kufua hewa tiba (oksijeni), hivyo kupunguza gharama za uendeshaji kwa hospitali hizo, pia kuziwezesha hospitali nyigine za halmashauri na vituo vya afya kuifanikisha .

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dk. Dorothy Gwajima, alipozuru hivi karibuni kukagua mitambo iliyounganishwa kwenye wodi za wagonjwa mahututi na watoto katika Hospitali ya Rufani Mkoa Dodoma, anasema mradi umewezeshwa na serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Dunia.



Waziri Dorothy Gwajima. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema, hadi sasa imefungwa kwenye hospitali za rufani za mikoa saba, akizitaja kuwa; Dodoma, Mtwara, Manyara, Mbeya, Amana, Geita na Songea, huku wizara yake ikiwa katika hatua za ukamilishaji wa kufungia hospitali zote za rufani za mikoa nchini.

"Mitambo hii imefungwa kwa gharama isiyopungua Sh. bilioni 1.4 kila hospitali na inalenga kuzalisha mitungi 200 ya hewa hiyo kwa saa 24 na kila mtambo unayo sehemu ya mabomba yenye mita 400 yanayosafirisha hewa hii," anasema.

:"Pia mitungi 73 imenunuliwa pamoja na mitambo hii kwa hiyo, haya ni mapinduzi makubwa," Waziri Gwajima anausifu uongozi wa Hospitali hiyo ya Dodoma, kwa kukamilisha ufungaji mitambo na kuanza kutoa huduma kwenye wodi za wagonjwa mahututi (ICU) kama ilivyopangwa.

Pia, ni huduma iliyofikishwa kwenye wodi za watoto na zimeunganishwa sasa kwenye vitanda 78, kutoka vitanda 10 vya awali, kufanya jumla ya vitanda 88 kupatiwa huduma hiyo hospitalini.

"Hatua hii itapunguza kwa kiwango kikubwa gharama za kuhudumia mgonjwa mwenye uhitaji wa hewa hii. Wito wangu tuitumie vizuri na kuzingatia na kuhakikisha matengenezo kinga yanafanyika kwa ufanisi," anahimiza.

Dk. Gwajima anasema, uwekezaji huo umeweza kujibu pengo la kipindi cha mlipuko wa ugonjwa Covid-19 ulioripotiwa nchini mwezi Machi mwaka jana, hata kusababisha ongezeko la mahitaji ya hewa ya oksijeni kwa wagonjwa, gharama zake zikipanda maradufu.

"Niwapongeze sana waganga wafawidhi wa hospitali za rufani za mikoa, kwa kuja na wazo hili la kufunga mitambo hiyo kwenye hospitali zetu.

"Hivyo, tutaweza kusaidia hospitali za wilaya na vituo vya afya na kuwapunguzia matumizi ya fedha za kununua Oksijeni. Haya ni mapinduzi makubwa kwa serikali yetu," anasisitiza Dk. Gwajima

Anataja kuwa ni namna inayosaidia kuepuka magonjwa ya kuambukiza ambayo yaliikumba nchi na mataifa mengine na anawataka waganga wakuu wa mikoa na wafawidhi kwenye hospitali za rufani, kuendelea kutoa elimu kwa umma kutumia vyombo vya habari, zikiwamo redio jamii katika maeneo mbalimbali nchini.

"Serikali kupitia sekta ya afya, kwa kushirikiana na wadau wake nchini, iko makini kufuatilia kinachoendela duniani na kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama na imara katika kudhibiti milipuko ya magonjwa mbalimbali, ukiwamo huu wa covid-19," anasema.

Dk. Gwajima anawakumbusha wadau, wataalamu, pamoja na wananchi kuendelea kuchukua tahadhari za kuelimishana kila mara, kinga na namna ya kudhibiti magonjwa mbalimbali, ikiwamo covid-19.

Hatua za tahadhari zinaanzia kuepuka hofu, pia kuimarisha tabia ya kunawa mikono kila mara, kwa kutumia maji safi tiririka na sabuni, kufanya mazoezi, kupata lishe au vyakula vya mboga kwa wingi na matunda.

Mengine yanayoshauriwa, yanajumuisha matumizi ya tiba asili, kuepuka misongamano isiyo ya lazima na anayejishuku ugonjwa, anapaswa kuwahi kwenye vituo vya tiba.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa Dodoma Dk. Ernest Ibenzi, amesema wanatarajia kufunga mitambo ya kujaza hewa tiba, ili kuweza kusaidia vituo vya afya vilivyo jirani na kusambaza huduma hiyo kwenye hospitali nzima.

AFYA

# Mkoa Manyara unavyong'ara katika operesheni chanjo wajawazito, watoto

## •Waratibu wajigamba kumudu malengo

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

WAKATI ni siku chache zilizopita dunia imeadhimisha Wiki ya Chanjo Duniani, Mkoa wa Manyara unatamka kwamba, imekuwa na tija kwa kuwahamasisha wazazi kuwaleta watoto katika mamlaka za afya wakapatiwe chanjo.

Mratibu wa Chanjo mkoani hapa, Suleiman Manoza, anasema wanawalenga watoto waliozaliwa hadi kufika umri wa miaka mitano, wakiamini inawezekana mzazi ama kwa kujua au pasipo kujua, hakumpeleka mtoto wake kupata chanjo.

Anasema, kimkoa hawana bajeti ya kufanya maadhimisho hayo, bali kinachofanyika ni kutekeleza majukumu yao kwa kutoa elimu ya kwenda kwenye vituo vya afya kupata huduma tajwa.

HALI ILIVYO

Mtaalamu huyo anajinasibu kwamba, hali ilivyo sasa siyo mbaya, kuna chanjo za kutosheleza wahitaji kimkoa, akitaja hitaji la mwaka huu ni kuchanja watoto 73,672.

Anasema, kati ya Januari na Machi mwaka huu wameshawachanja watoto 15,808 ambao ni sawa na asilimia 83 ya malengo kwa kipindi husika na kunafanyika chanjo tatu, zikipewa umuhimu.

Mratibu huyo anasema hufanyika pale mtoto anapozaliwa kufikisha wiki sita, anatakiwa kupatiwa chanjo ya kwanza na anapofika umri wiki 10, anatakiwa kuchanjwa, hali kadhalika wiki ya 14 ana chanjo ya tatu.



Mratibu wa chanjo wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, James Mleli, akiwa amempakata mtoto anayechanjwa katika Kituo cha Afya Magugu. **PICHA: JALIWASON JASSON.**

"Mtoto akikamilisha chanjo tatu, Wizara ya Afya ndio inayotambua kuwa amechanjwa," anasema, huku akitaja madhara husika ni magonjwa kama surua, nimonia, kuharisha, dondakoo, homa ya ini, polio, kifua kikuu, pepopunda, kifaduro, homa ya uti wa mgongo na kichomi.

Namna ya kufanikisha hoja hizo, anasema ni kuwapo namna ya kuwabana wazazi wasiopeleleka watoto wa kwenye huduma ya chanjo, ingawaje hakuna sheria mahsusi inayowabana wanaoshindwa kuwapatia chanjo.

"Sayansi inasema, ukiwachanja watoto 100 ni asilimia 85 wanakingwa, ila asilimia 15 hawapati kinga. Ndio maana wizara huwa inaandaa kampeni, ili zisaidie kutafuta ile asilimia 15 inayobaki," anasema.

Anasema asilimia 15 inayobaki, huwa wanahisi hawajapata chanjo, ndio maana wizara inafanya kampeni kuwasaidia watoto ambao chanjo hazijawanufaisha.

Mtaalamu huyo anasema faida kubwa anayopata mtoto akichanjwa ni kumkinga na magonjwa, akisema mwaka jana walifanikiwa kuwachanja watoto kwa asilimia 98.

Anasema, kuna wakati chanjo wamekuwa wakizikosa kutokana na uhaba wa majokofu, mengi yalikuwa ya kizamani na kuchoka, lakini sasa tatizo limetatuliwa

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, yanayotumia nishati ya jua.

**KWA WAJAWAZITO?**

Mratibu huyo wa chanjo ya 'tatenus' kwa wajawazito, anasema mwaka huu wameweka malengo ya kuwachanja wajawazito 79484 na kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu, walishachanjwa wajawazito 10322 sawa na asilimia 12 ya walengwa wote, wakinuia kuwaweka salama dhidi ya maradhi hayo, wakati wa kujifungua.

Anasimulia kwamba, kinamama wanaojifungua nyumbani wanatumia mbinu ya kuwapaka watoto wao kinyesi cha ng'ombe kitovu ili kikauke, kitu kinachoweza kumsababishia madhara makubwa mtoto na mbadala sahihi, ni chanjo inayomuweka salama mtoto.

Anasema mama mjamzito anatakiwa achanjwe kwa awamu mbili, ya kwanza anapoanza kliniki na chanjo ya pili anatakiwa baada ya mwezi mmoja, ambayo kimsingi haina kinga ya kudumu, ila pili ndio muhimu.

Manoza anasema, ni aina ya chanjo anayofanyiwa mjamzito kuanzia miaka 15 hadi 49, akipatiwa chanjo tano inayodumu kuwa kinga yake kwa miaka 20.

**KUTOKA BABATI**

James Mleli, Mratibu wa Chanjo wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, anasema maadhimisho ya wiki ya chanjo yanalenga watoto waliokuwa wamekosa.

Anasema wanatoa elimu kwa wazazi, ili kuwapa hamasa ya kuwapeleka watoto kupata chanjo, wale waliokuwa hawajashiriki chanjo, lengo kitaifa ni asilimia 95 kwa chanjo aina zote.

Mlelin anasema, halmashauri yao imefanikisha asilimia 95 ya malego yao ya chanjo kwa kipindi cha kati ya Januari hadi Machi mwaka huu na kilichowasaidia kuvuka hatua hiyo, ni kuwapo kliniki za mikoba (kliniki tembezi).

Ni aina ya kliniki inayoelezwa, kuwezesha watoto kuwapo kila siku kwenye vituo vya kutoa huduma za afya na kwa mwaka huu Babati wanawalenga kuwachanja watoto 14987, ilhali hadi kufika mwezi Machi wamefanikisha asilimia 90 ya lengo lililokuwapo la chanjo tatu za awali.

**KAULI ZA WANANCHI**

Mkazi wa Babati, Charles Mwombeki, anasema utoaji chanjo, umesaidia kwa kiwango kikubwa kuwaepusha watoto wao, kutoka hatari na magonjwa ukilinganisha na zamani, wengi waliugua na kudhurika na maradhi surua.

Mwenzake, Daghailoy Hashimu, anaishukru serikali kwa kuimarisha kitengo cha chanjo, zinazopatikana katika ngasi zote za makazi hadi vijijini.

Hashimu, anasifu mafanikio ya mamlaka hayo ya kiserikali, imefanikiwa kutoa chanjo kwa kila mwananchi, huku wakiwa na uelewa sahihi wa namna ya kumpatia mtoto wake chanjo na hakuna mzazi anayepuuza chanjo.

Mkazi mwingine wa Majengo Mapya- Babati, Rehema Donatus, anasema elimu ya kuwachanja watoto, huwa inaanzia nyumbani kwa wazazi, kwa kuwa kila mzazi alishakariri kuwa mama alishapata mtoto ni lazima apate chanzo zote zinazoshauriwa kitaalamu.

Rehema anasema ana watoto watano na hakuna kati yao, ambaye hakupata chanjo, wazazi wengi wanajua umuhimu wake.

Mkazi wa Mtaa wa Nyunguu Godbetha Sanka, anasema uelewa walio nao kinamama kwenye chanjo, huku akisema ni kinga kwa watoto, jambo linalompa hiari kuliafiki.

Mkazi wa Mtaa wa Ngarenaro, Justa Bahati, anasema wengi wanaichukulia chanjo katika sura ya tiba kwa mtoto ambayo hakuna wa wa kuipinga.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ya mwaka 2015, watoto waliochanjwa walikuwa asilimia 93 wakati takwimu za wizara sasa ni asilimia 96.

Shirika la Afya Duniani (WHO), linakadiria kati ya watoto 10 duniani, mmoja alikosa chanjo ya kuokoa maisha dhidi ya magonjwa kama surua, dondakoo na pepopunda.



Baadhi ya kinamama waliopeleka watoto katika kliniki ya Mrara kupatiwa chanjo, kwenye uzinduzi wa Wiki ya Chanjo uliofanyika Aprili mwaka 2017, katika Hospitali ya Mrara. **PICHA: MTANDAO**

AFYA

# Unajua msamaha unakuepusha na mlolongo wa maradhi mwilini?



Picha zinazoonyesha watu wakiwa katika hisia tofauti. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Martha Mwasyeba**

INAELEZWA kijamii, utoaji msamaha umebaki kuwa mtihani mgumu kibinadamu. Ila inapotekelezwa mafanikio yake yanabeba majibu bora kiafya.

Hali iliyoko ni kwamba asilimia kubwa ya wanaoishi na chuki, vinyongo, hasira kwa kukosewa na ndugu au jamaa zao, wanaangukia kuathirika kiafya, kwa sababu wanabakiwa na mengi mioyoni pasipo kujua hatari inayowakabili, ikiwamo kupatwa na maradhi hatari.

Mwandishi wa kitabu 'Siri ya Msamaha,' Dk. Stephen Kadilo, Padre wa Jimbo la Katoliki Shinyanga na bingwa wa magonjwa ya kinamama, anayetumikia Hospitali ya Rufani Mtakatifu Francis, Ifakara ana dokezo lake kitaalamu.

Anaanza na tafsiri ya Shirika la Afya Duniani (WHO), kwamba 'afya njema' inabeba tafsiri mtu kukamilika kimwili na kiakili, pasipo ugonjwa au udhaifu .

"Hisia kali ndani ya nafsi zetu zinaweza kuwa chanzo cha majeraha makubwa, kwa akili na miili yetu," anasisitiza Padre Dk. Kadilo, anayefafanua hasira, chuki na huzuni zinavyoyowafika wengi kuwakosesha afya njema.

**HILO LINATOKEAJE?**

Mtaalamu, Dk. Ann Landers, anasema mwenye hasira na chuki iwe muda mrefu au mfupi, ni mgonjwa anayehitaji dawa ya msamaha. Anaendelea: "Chuki ni kama tindikali inayoharibu kifaa kilichohifadhiwa na huharibu chombo ambacho kimemiminiwa."

Dk. Landers anaeleza msamaha kwenye jamii ni muhimu na hitaji la lazima na afya ya wengi haiko salama, kwa sababu ya vinyongo na hasira vinayopaswa kuachiwa kwa msamaha.

Bingwa wa magonjwa ya akili nchini Marekani, Dk. Karl Augustus Menninger, ana maoni ya kitaalamu anayoyaeleza: "Kuomba na kupokea msamaha ni tiba dhidi ya magonjwa ya akili.

"Kama wagonjwa kwenye hospitali za magonjwa ya akili wangeweza kushawishika, maovu yao yamesamehewa asilimia 75 (robo tatu) ya wagonjwa hao wangetoka hospitali siku inayofuata, wakiwa wamepona."

Daktari Menninger, anakiri kuwapo ugumu wa misamaha unaobebwa na ushahidi wa kuenea magonjwa ya saratani, kisukari, kiharusi, vidonda tumbo, uoni hafifu na sonona.

Anataja; kinyongo, hasira, chuki na hisia za kulipiza kisasi, ni mlango unaomfanya mtu kushindwa kutengeneza kinga mwilini.

Mtaaluma huyo anaeleza kwamba kitabibu hasira ni hatari kwa afya ya mwili, ingawaje bado haijafahamika kwa wengi, mtazamo unaoafikiwa na mwandishi wa kitabu 'Nimeamua Kusamehe.'

Pia, kuna baadhi ya utafiti unaoanika kwamba wenye magonjwa kama shinikizo la damu, kipanda uso, vidonda tumbo, kuzubaa au bumbuazi, kuchanganyikiwa na homa za kila mara, mzizi wake uko moyoni, hasa katika dhana ya kutosamehe.

**HASIRA INAVYOATHIRI**

Kwanini hasira inadhuru? Kiafya, binadamu anapokuwa katika mazingira hatari, anatawaliwa na wasiwasi, mihemko, woga au ugomvi. Hapo, mwili wake unazalisha homoni inayoitwa 'Adrenaline' au 'Epinephrine.'

Hiyo inauwezesha mwili wake kupambana na kukimbia hatari inayomfika aliko na ndio chanzo cha homoni hiyo kuitwa 'fight and flight hormone' au 'homoni mpiganaji.'

Adrenaline inazalishwa kuanzia iliko figo za 'Adrenal Glands', ambazo ni muhimu kusaidia usalama wa mwili, lakini ina madhara lukuki inapobaki bila sababu ya msingi.

Homoni Adrenalinen inafanya kazi, pale inapofikia vipokezi vitwavyo 'alpha' (ndani ya mishipa ya damu) na vipokezi 'beta' (kwenye moyo).

Hivyo, huwa vinafanya kazi na vipokeo vya insulini iliyozalishwa kwenye chembehai aina ya 'beta' (Beta Cells) zilizopo kwenye kongosho, sehemu ijulikanayo kwa jina la kitaalamu 'Islets of Langerhans.'

**HOMONI INAVYOFANYA KAZI**

Homoni huwa inaungana na vipokezi vya za kumen'genya 'molekyuli' kubwa za sukari, kisha zinaungana na vipokezi vya chembehai kwenye misuli ya mapafu, kuwezesha kupumua kwa kasi zaidi.

Ni hali inayosisimua chembehai moyoni, mapigo yake yakiogezeka kasi. Hapo, inashitua mishipa ya damu inayosinyaa kuelekeza damu nyingi kwenye misuli mikubwa tu.

Hapo inasisimua chembehai za misuli iliyoko chini ya ngozi, kuufanya mwili utoke jasho, kupooza joto lililoongezeka.

Ni hali inayojitokeza pale mwili umedhamiria kutoa homoni hiyo kwa lengo zuri la kujiokoa na adui, maana wingi wa sukari huufanya mwili uwe na nguvu nyingi kuliko kawaida.

Adrenalini, inapozalishwa kwa mwitiko wa kila siku wa huzuni, woga kinyongo au hasira, nao unasababisha madhara makubwa mwilini.

Hilo linajumuishwa na akili iliyojaa mawazo, woga, wasiwasi, hasira na mhemko, hata kusababisha kuzalishwa adrenalini kwa namna ileile. Nini hali inayochangia kuzalishwa homoni nyinginezo inayohusiana na mfadhaiko zijulikanayo kwa majina 'cortisol' au 'linguine stress hormone.'



Mathalan, mtu anapofikiria ugomvi uliotokea, manyanyaso au dhana ijayo, ina kawaida ya kusababisha uzalishaji homoni hizo mbili kwa wingi.

Hapo inaongeza nguvu ya ziada mwilini pasipo jukumu lolote. Zao la homoni hizo, humfanya mtu anakuwa mwepesi kukasirishwa, anakosa usingizi na kwa baadhi ya watu kichwa kinauma au kipandauso na anachoka pasipo kutumika nguvu yake mwilini.

**HAMU YA KULA?**

Hamu ya chakula inaoongozwa na ubongo, sehemu inayoitwa kitaalamu 'kituo shibe au 'kituo kina'. Hapo hakutakuwapo mwaliko wa ubongo kuagiza mtu ama ahisi njaa au ale chakula, kwani muda wote anajihisi ametosheka, hana hamu ya kula.

Huo ndio wakati tindikali inapoongezeka tumboni na kukwangua utando ndani ya utumbo, ikiambatana na kumwagika nyongo nyingi kwenye utumbo mwembamba uitwao 'duodenum' na inapoongezeka kwa msaada wa homoni iitwayo 'Cholecystokinin' na 'Sekretin', inajenga sumu inayosababisha vidonda tumboni.

Katika hilo likiendana na mtu anakesha macho muda mrefu na analala muda mfupi, ametawaliwa na mawazo yasiyoisha, anaishia kujijengea hali ya kuzubaa na bumbuazi.

Wanasaikolojia wanatafsiri hali hiyo ni maradhi sonona au msongo wa mawazo. Mtu anajenga tabia ya kukasirika, anajichukia, anajihisi hafai, anajitenga na wengine, akiwa amekata tamaa.

Matokeo yake panashuhudiwa matukio ya watu ama anajidhuru au anatamani kujidhuru. Hiyo ndio sababu ya maana, katika hilo, wanasaikolojia wanashauri, kada hiyo ya jamii isikilizwe kwa huruma na hisia kuu.

Mara zote wataalamu wanadumu kusimamia kwamba jamii hiyo si zao la laana, bali wanatibika kuanzia ngazi ya ushauri sahihi.

Kisukari? Utendaji wa ini unapolazimishwa tofauti na kawaida huzalisha sukari mwilini isiyo na kazi, huku vipokezi vya insulin vinazuia utendaji kazi kadri mwili ulivyoumbwa na ndio chanzo cha ugonjwa wa kisukari.

Pia, moyo unapokuwa na kasi kubwa ya mapigo kwa muda mrefu, kutokana na wingi wa homoni aina ya adrenalini inayoletwa na hasira, inaifanya iongeze kasi ya kusukuma damu isivyo kawaida na kwa muda mrefu.

Huo ndio unakuwa mwanzo wa ugonjwa wa moyo au unaweza kupanuka na kushindwa kusukuma damu ipasavyo kufika sehemu zote za mwili.

Kuna wakati inatokea msukumo wa damu unakuwa juu zaidi, hata kumsababishia mtu kiharusi.

Hapo ndio dawa ya kusamehe ina mchango mkubwa, kufuta mlolongo wa madhara mwilini kwa binadamu.

AFYA

## KINACHOJIRI SHINYANGA & SINGIDA...

# Mratibu utapiamlo anavyotoa darasa kutumia uzoefu wa kumudu ya kwake




Mratibu wa Lishe na Jinsia, kutoka Taasisi ya Sekta Binafsi ya Kuendeleza Sekta ya Horticulture Tanzania (TAHA), Salome Stephen, alipotoa elimu ya lishe kwa kikundi cha wanawake vijana, mkoani mkoani Shinyanga. **PICHA: SHABAN NJIA**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

UTAPIAMLO ni miongoni mwa shida za kiafya zinazoikabili Tanzania, hata kupatikana watoto wenye udumavu na utapiamlo kwa kiwango kikubwa, chanzo kikihesabiwa ni lishe duni hasa katika baadhi ya maeneo ya vijijini.

Katika kukabili adha hiyo, kuna juhudi za moja kwa moja kama vile huduma za kiafya, pia nyenzo elimu zimekuwa zikitolewa.

Hapo kuna nguvu ya mashirika mbalimbali kwa kushirikiana na serikali na zimekuwa zikiingilia kati hilo kutafuta jibu la kuumaliza utapiamlo.

Lishe duni kwa mtoto inachangia awe na kimo kifupi kisichoendana na umri wake, huku sababu nyingine zinatajwa ni pale mtoto anapougua.

Ugonjwa wa mtoto kudumaa, kuna wakati inamwachia athari zisizorekebishika katika maisha yake, hata kama baadaye atapewa lishe bora, tayari mwili wake utakuwa umedumaa na kushindwa kupokea marekebisho mapya mwilini.

Kipindi kinachotajwa hatari kiafya kwa mtoto ni siku 1000 za kwanza za uhai wake, sawa na wastani wa miaka miwili na nusu.

Hapo ndipo inatajwa asasi binafsi inayojishughulisha na kuendeleza kilimo cha bustani nchini, iitwayo TAHA. Hiyo imejikita katika utoaji elimu ya kuandaa chakula chenye lishe bora, kwa kutumia vyakula vinavyopatikana kirahisi, mlengwa mkuu ni mjamzito na mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano.

Kupitia mradi wake uitwao "Kutambua Usawa wa Kijinsia kwa Kuwawezesha Wanawake na Wasichana" unaangukia mikoa ya Shinyanga na Singida.

Shinyanga, TAHA inatekeleza mradi huo katika Halmashauri ya Msalala kata za Shilela, Segese na Lunguya huku mkoani Singida katika Halmashauri ya Wilaya Ikungi, katika katika vijiji vya Kipumbuiko, Mnang'anana, Sepuka, Irisya na Muyu.

Ni mradi unaoenda sambamba na utoaji elimu ya lishe, kwa vikundi vinne vya Halmashauri ya Msalala na vikundi 12 Halmashauri ya Ikungi.

Hapo lengo ni kuwapatia uelewa wananchi kuhusu masuala ya lishe na lishe sahihi, ili kuukwepa udumavu kwa watoto.

### MRATIBU MRADI

Salome Stephen, Mratibu wa Lishe na Jinsia kutoka TAHA, anasema mradi ulianza mwaka jana na inatarajiwa kukamilika mwaka 2023 kwa kuwafikia wanufaika 437 walioko katika vikundi 16 katika halmashauri za Msalala, Shinyanga na Ikungi ya Singida.

Mratibu huyo anasema, mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano, kila siku anatakiwa kupata milo mitano, katika mgawanyiko; milo mikubwa mitatu; na milo midogo miwili, ambayo kwa ujumla, inamsaidia mtoto kukua vizuri, akiondokana na shida ya utapiamlo.

Anasema shida kuu iliyoko, kinamama wengi hupata ujauzito pasipo kutambua namna bora ya kuandaa lishe zao wakati wa ujauzito, hali inayowafanya wajifungue watoto wenye uzito pungufu na hawana damu.

Salome anataja kasoro walio nayo kinamama, ni kwamba wengi waakula chakula kwa lengo kushiba, pasipo kufuatilia afya ya kimwili na kiakili, matokeo yake wanaozaliwa wanashindwa kutunza kumbukumbu, ikiwamo masomoni.

### UNYONYESHAJI ULIVYO

Pia mratibu huyo anasema iwapo tabia ya baadhi ya kinamama wanaonyonyesha, wanaacha kufanya kwa madai ya kulinda maumbo yao, huku wakiwa hawatambui ni namna inayokaribisha hatari ya magonjwa kama kansa ya matiti na saratani shingo ya mlango wa kizazi.

Salome anasema, umuhimu wa mtoto kunyonya unakoma baada ya kutimu siku 1000, lakini kinyume chake kuna baadhi ya kinamama wanawaachisha kunyonya watoto wao baada ya kutimiza mwaka mmoja au kupata ujauzito mwingine.

Ushauri wake ni kwamba, hata mama anapopata ujauzito mwingine huku ukiwa na mtoto mdogo, ni vyema unamwanzishia mtoto maziwa ya ng'ombe na unatakiwa kumpatia wakati wote, ikiwamo usiku.

Hapo kunatajwa ni suluhisho la madhara kwa mtoto kama vile kupata matege na kukakamaa ubongo na mifupa yake.

"Mimi nilipata ujauzito mwingine huku nikiwa na mtoto mdogo na bado alikuwa anahitaji kunyonya. Ila nilimwachisha kunyonya na kumwekea bili ya maziwa na kumnywesha usiku na mchana na alikuwa na afya ya kutosha," anasema.

Salome anaendelea: "Hii inasaidia kuondoa tatizo la udumavu....tusiwatelekeze watoto wetu tunapopata ujauzito mwingine.

### WANENAVYO WADAU

Diwani wa Kata ya Lunguya katika Halmashauri ya Msalala, Benedictor Manwari, anasema wamekuwa wakiwahamasisha wajawazito kuhudhuria kliniki kipindi chote cha ujauzito na kujifungua katika vituo jirani vya afya.

Anasema lengo la kuwahamasisha kujifungua katika vituo vya afya, ni kumpatia elimu ya maandalizi ya chakula chenye lishe kwa watoto wao wanaokuwa wamejifungua, ili kuendelea kupambana na tatizo la udumavu au utapiamlo.

"Sehemu za vijijini kunahitajika elimu ya lishe kwa kinamama wajawazito na wanaoendelea kulea. Hii ndio sababu inayonifanya kwenye mikutano ya hadhara kuwaalika wataalamu wa lishe, ili kutoa elimu kabla ya mkutano kuanza," anasema.

Kwa mujibu wa diwani huyo, kwenye mikutano ya hadhara, wamekuwa wakiwaalika wataalamu wa lishe kutoka makao makuu ya wilaya wanaotoa elimu kuhusu namna ya kuandaa lishe bora kwa watoto, ikiwa sehemu ya mapambanio kuukabili udumavu.

Christina Stephen, Mwenyekiti wa Wanawake Vijana kutoka Kata ya Lunguya, anasema kukosekana elimu ya lishe, kunasababisha chakula kinaandaliwa kienyeji na kuwalisha watoto lishe duni, ikiangukia athari za mwili na akili kwa watoto.

Anasema, awali kabla ya kupatiwa elimu alikuwa akiwalisha watoto mlo duni, hivyo elimu imemnengua kutoka athari hiyo, sasa akiandaa mlo wa watoto unaangukia wasifu mlo bora, wenye makundi matano aliyojifunza.

Naye mkazi wa kijiji cha Marito, Leah Mathius, anasema ukosefu wa kipato cha uhakika ndani ya kaya, ni chanzo kingine kwa baadhi ya familia kushindwa kupata mlo bora kwa watoto wao, ambao unaelekezwa na wadau lishe.



# Bil. 5/- kuharakisha kasi ya maji Jiji la Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amesema kazi ya uboreshaji wa haraka wa hali ya upatikanaji maji katika Jiji la Dodoma na Wilaya ya Chamwino imeanza kwa serikali kutoa Sh. bilioni tano kwa ajili ya kazi hiyo.

Aweso aliyasema hayo jana kwenye ziara ya Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ya kukagua hali ya upatikanaji wa maji katika maeneo hayo kutokana na kuwapo kwa ongezeko la watu baada ya serikali kuhamia Dodoma. "Visima 10 tayari vimeshachimbwa vikiwamo vitatu vikubwa na Wizara ya Maji imeanza kutathmini mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi mkoani Dodoma, na pia mradi wa bwawa la Farkwa nao upo kwenye hatua ya kuanza utekelezaji wake, lengo ni kuhakikisha Dodoma inakuwa na maji ya kutosheleza," alisema Aweso.

Aidha, alisema kwa sasa jiji hilo lina ongezeko la watu na hayo maboresho ni ya haraka na mkakati mwingine ni kuhakikisha wanatoa maji kutoka ziwa hilo kuja Dodoma.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Dk. Christine Ishengoma, alisema kamati hiyo imeridhishwa na hatua zilizochukuliwa na wizara pamoja na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) za kuongeza uzalishaji maji.

"Tunaamini kuwa tutapata maji ya kutosha katika Jiji la Dodoma na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alitaka miongoni mwa miradi inayotekelezwa ni ujenzi wa tangi la kuhifadhia maji Buigiri lenye uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo milioni 2.5 ambazo zitahudumia Wilaya ya Chamwino na eneo la Ikulu. "Mradi huu ulikuwa na thamani ya Sh. bilioni 2.5, lakini umetekelezwa kwa Sh. milioni 998 kwa maelekezo ya wizara kwamba tuhakikishe tunapunguza gharama za utekelezaji wa miradi na tumefanikiwa kwa kuwa tupo asilimia 98 ya utekelezaji wa mradi huu wa tangi," alisema.




Wakazi wa Jiji la Dodoma, wakimwangalia mtu aliyelala chini (kushoto), baada ya kugongwa na Bajaji, katika Barabara ya Sido, eneo la Uhindini, jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Ummy awapa angalizo watumishi watakaoharibu

**Na Mwandishi Wetu,** CHEMBA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amesema mtumishi yeyote atakayeharibu katika kituo chake cha kazi hataruhusu kuhama, bali atamwajibisha akiwa katika kituo chake cha kazi.

Waziri Ummy alitoa kauli hiyo jana kwenye ziara yake wilayani Chemba mkoani Dodoma ya kukagua miradi ya maendeleo na kuzungumza na Kamati ya Fedha pamoja na Menejimenti ya Halmashauri hiyo.

"Sitaruhusu mtumishi aharibu Chemba kisha ahamishiwe Kongwa, niwahakikishie kuwa nitamshughulikia akiwa hapa hapa Chemba na nikibaini ana hatia nitamchukulia hatua stahiki," alisema.

Alibainisha kuwa kuna baadhi ya watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wamezoea kufanya ubadhirifu wa miradi ya maendeleo haswa ya Elimu, Afya na Barabara anaomba uhamisho kukwepa tuhuma.

"Wakishaona mradi haujakamilika au unatuhuma hizi na zile anahama sio wakati wa uongozi wangu hakuna atakayehama kukwepa tuhuma, na hapa Chemba wote waliohama sababu ya kutokukamilisha miradi ya maendeleo kama ujenzi wa hospitali ya wilaya watarudi kuja kujibu tuhuma zao," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Ummy aliwataka wakuu wa mikoa, makatibu tawala mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri kuendelea kuchapa kazi kama awali na sio kukaa kusubiria uteuzi.

"Hali inayoendelea kwa viongozi hawa haileti afya, wengine hawafanyi kazi eti wanasubiria mkeka, hamuoni kuwa mnaonea wananchi kupata haki yao ya msingi ya kuhudumiwa?" Alihoji.

Aliongeza: "Kipindi hiki mnatakiwa kuendelea kuchapa kazi kama kawaida kwani wananchi wanahitaji kuendelea kuhudumiwa, suala la mkeka unakuja lini hilo ni kuliachia mamlaka, ninyi chapeni kazi."

Aliwasisitiza viongozi hao kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, huku wakimtanguliza Mungu mbele ambaye ni mpangaji wa kila jambo.

## Wanaojifanya maofisa TAKUKURU waonywa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoa wa Dodoma, imewatahadharisha wananchi kuhusu matapeli wanaojifanya ni maofisa wa taasisi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na utapeli huo, Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, alisema, katika siku za hivi karibuni limeibuka wimbi la matapeli wanojifanya ni maofisa wa taasisi hiyo.

Alisema kuwa watu hao wamekuwa wakitumia mwamvuli wa taasisi hiyo kuwaita watu kwa madai wanawafanyia uchunguzi na baadaye wanawatapeli fedha zao.

Alisema wananchi wanatakiwa kuwa makini na watu hao kwani TAKUKURU haifanyi kazi kwa utaratibu huo.

"Kuna wimbi la watu wanaojifanya maofisa wa TAKUKURU linaendelea kuishika kasi katika maeneo mbalimbali watu wanapigiwa simu wanaambiwa waje katika ofisi za zetu za makao makuu wakati siyo kweli," alisema.

"Uchunguzi wetu umebaini wengi wao hawapo Dodoma, hii inaonyesha wanawatisha watu wanaowaita na kujifanya wana taarifa zao zina shughulikiwa hapa TAKUKURU wakati si kweli, jamii kuweni makini," alisema Kibwengo.

Alifafanua zaidi ya kuwa watu hao wamekuwa na tabia ya kujifanya wanampigia mlengwa simu baada ya mazungumzo ya awali wanapiga tena na kujifanya wanamuunganisha na bosi wao na huyo bosi kuanza kumweleza kuhusu uchunguzi unoendelea dhidi yake.

"Unakuta mlengwa anaunganishwa na mtu anayejifanya kamanda anamtaja na jina kumwambia hapa kuna suala lako inabidi uje Dodoma, lakini kama unataka msaada," alisema Kiwengo.

Alisema kwa wale wasiojua utaratibu wanaishia kutapeliwa fedha zao na wengine wanakuja mpaka Dodoma.

"Niwakumbushe wananchi kwamba huduma za TAKUKURU hazilipiwi na haimwiti mtu kwa njia hiyo lazima utapewa karatasi maalum ya wito, au kama upo nje ya Dodoma, wenzetu waliopo katika mikoa na wilaya watawasiliana na wewe, lakini siyo kwa utaratibu huo hatupigii mtu simu halafu tunaanza kujadili uchunguzi unaofanyika dhidi yako, hakuna kitu kama hicho msikubali kuibiwa," alisema Kibwengo.

Hata hivyo, aliwasisitiza wakazi wa jijini Dodoma kuendelea kutoa ushirikiano wa utoaji taarifa pale wanapoona kuna viashiria vya rushwa ili zifanyiwe kazi kwa ufasaha.





## Waomba sera kumlinda mwanamke kwenye kilimo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imeshauriwa kuandaa sera itakayomlinda mwanamke anayeshiriki kwenye shughuli za kilimo, kunufaika na rasilimali zilizopo na kujikwamua kiuchumi badala ya kuendelea kuwa tegemezi katika jamii.

Mkurugenzi wa shirika lisilokuwa la kiserikali TGNP- Mtandao, Lilian Liundi, alisema ni wakati sasa wa kuunda sera itakayomlinda mwanamke anayejishughulisha na kilimo ili afurahie maisha.

Alisema wanawake hasa waishio vijijini hawahusishwi na wenzi wao kupanga matumizi msimu wa mavuno na kwamba uwapo wa sera itayomlinda mwanamke ili kupata haki ya kufanya uamuzi katika mavuno hayo itasaidia kulinda heshima na kushiriki kupanga matumizi.

"Tunahitaji sasa sera ya kutuongoza kuhakikisha wanawake wanapewa nafasi ya kufanya maamuzi ndani ya familia pindi msimu wa mavuno unapowadia ukilinganisha na ilivyo sasa ambapo wanaume wengi huku Mbeya Vijijini ni wababe hawashiriki wenzi wao matokeo yake hutafuta michepuko," alisema Liundi.

Alisema unyanyasaji wa kiuchumi hasa msimu wa mavuno hurudisha nyuma jitihada za mwanamke kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa sababu ya kukosa fedha na kukatishiwa tamaa na waume zao.

Aliongeza kuwa kampeni ya 50 kwa 50 ambayo inapigiwa kelele na wadau mbalimbali lazima ianzie ngazi ya chini kwa sababu wanawake wengi hawajiamini kugombea kutokana na kukosa fedha na ukizingatia wengine ni wakulima, lakini wanapovuna mazao wanakuwa hawana uamuzi.

Mwenyekiti wa vituo vya Taarifa na Maarifa katika Wilaya ya Mbeya, Flora Mlowezi, alisema wanawake na wanaume wana haki ya kumiliki rasilimali zao kwa usawa bila ubaguzi kwa kisingizio cha jinsia.

Mlowezi alisema tayari wameanza mkakati wa kutoa elimu kwa jamii hususani wanaume kuacha tabia ya ubabe na mabavu wakati wa mavuno badala yake washirikiane na wenza wao katika kufanya maamuzi ya namna watauza mavuno yao.

Kiongozi wa kimila kutoka kabila la Wasafwa, Aron Mwazyunga alisema hatua ya kuwashirikisha viongozi wa jadi, masuala ya usawa wa kijinsia kutasaidia kuongeza idadi ya wanawake kupata nguvu na ujasiri kushiriki kwenye michakato mbalimbali ya uongozi.

# SUA kuwa kitovu cha kufikishia wakulima teknolojia

**Na Grace Mwakalinga,** KATAVI

SERIKALI inakusudia kukifanya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), Ndaki ya Mizengo Pinda iliyopo Halmashauri ya Mlele, mkoani Katavi, kuwa kitovu cha kuwafikishia wakulima nchini teknolojia bora za kilimo, ufugaji wa nyuki na utalii kwa lengo la kuhakikisha taifa linanufaika na sekta hizo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha SUA, Ndaki ya Mizengo Pinda iliyoko mkoani Katavi ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema wanalenga kuhakikisha chuo hicho kuwa kitovu za kuzalisha teknolojia za kisasa za kilimo ambazo zitasambazwa maeneo mbalimbali nchini.

Alisema teknolojia hizo zitajikita kuboresha ufugaji wa nyuki, utunzaji wa mazingira na kuhaulisha teknolojia nyingine ambazo zitahakikisha matakwa ya chuo na nchi yanafikiwa katika kuinua sekta ya kilimo nchini.

"Tumekuja hapa Katavi kwa lengo la kujadiliana na namna gani tuweza kuanzisha chuo hiki ambacho kimeanza mwaka jana nikiwa Mwenyekiti wa Bodi mikakati yetu ni kuhakikisha kinakuwa cha mfano kwa kuzalisha teknolojia bora za kisasa ambazo zitasaidia ufugaji wa nyuki na utunzaji wa mazingira na kuwanufaisha wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini," alisema Dk. Bucheyeki.

Mkuu wa Chuo hicho, Profesa George Mwamengele, alisema licha ya kwamba chuo hicho ni cha kitaifa, lakini lengo lake pia ni kusaidia jamii inayokizunguka kwa kuhakikisha wanapewa elimu na teknolojia za kisasa za kilimo.

Alisema licha ya mwamko mdogo wa vijana hususani kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, kujiunga na chuo hicho, lakini anaamini watakaosoma chuoni hapo watakuwa mabalozi wazuri wa kukitangaza kutokana na elimu bora ya kilimo watakayoipata.

Baadhi ya wanafunzi wa chuo hicho akiwamo, Anitha Lyaka, alieleza matarajio yake kuwa ni kupata ujuzi utakaomwezesha kwenda kuisaidia jamii yake kilimo bora.

Alisema wamefundishwa elimu ya ugani, matumizi ya teknolojia mbalimbali katika kilimo na namna ya kuwasaidia wakulima wanapopata matatizo kwenye mazao yao.

Silas Nanyala, alisema jamii bado inatumia njia za kizamani katika kuhudumia mazao yao na elimu atakayoipata chuoni hapo itamsaidia kuwaelimisha wakulima kuachana na mbinu za kizamani katika kuhudumia mazao badala yake kutumia teknolojia mpya ili kupata mavuno mengi.



Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa nchini (TANAPA), Godwell Ole Meing'ataka, akizungumza na walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari (hawapo pichani), kutoka maeneo ya hifadhi za Kitulo na Katavi kuhusu umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa hifadhi za taifa, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo yaliyofanyika juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# TANAPA kutoa mafunzo kwa walimu msingi, sekondari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limeanzisha programu ya mafunzo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari pamoja na walimu wa kawaida wanaozunguka hifadhi za Kitulo na Katavi ili kuwapatia elimu ya ujirani mwema na umuhimu wa utunzaji wa hifadhi hizo ili ziendelee kurithiwa na vizazi vya sasa na baadaye.

Hayo yalisemwa juzi na Kamishna Msaidizi wa uhifadhi nchini, Godwell Ole Meing'ataki, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo walimu wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari kutoka Hifadhi za Kitulo na Katavi.

Alisema walianzisha programu hiyo ili kuwafikia wanafunzi ambao bado hawatambui umuhimu wa hifadhi hizo na kupitia walimu wao watazilinda na kuzihifadhi.

Alisema, shule za msingi 23 na sekondari 13 kutoka mikoa ya Njombe, Mbeya na Katavi zimenufaika na elimu ya kujengewa uwezo wa masuala mbalimbali ya uhifadhi.

Alisema programu hiyo ambayo kwa sasa ni kama rasimu italeta mwitiko chanya kwa kuwa itawafikia walengwa moja kwa moja hususani wanafunzi ambao watakuwa mabalozi wazuri wa wazazi wao na jamii kwa ujumla.

"Tuliamua kuanzisha programu hii kwa wadau wa elimu baada ya kubaini kuwa licha ya kuwa na ujirani mwema na shule zinazozunguka hifadhi, bado hawana elimu ya kutosha ya umuhimu wa hifadhi zetu, kupitia mafunzo na shughuli mbalimbali tutakazozifanya, kupitia programu hii itasaidia kukabiliana na vitendo vya ujangili pamoja na uharibifu wa mazingira kuzunguka hifadhi," alisema Ole Meing'ataki.

Kwa upande wake, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi ambaye ni Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Kitulo, Theodora Aloyce, alisema programu hiyo itaongeza wigo wa elimu kwa wanafunzi kutambua umuhimu wa uhifadhi.

Alisema wanafunzi wakipata elimu hiyo itakaa vichwani mwao na kusimamia kikamilifu uhifadhi kwa kuwa watakuwa mabalozi wazuri wa wenzao na hata jamii.

Mkuu wa Wilaya ya Makete, Veronica Kessy, aliwaomba askari wa TANAPA katika Hifadhi ya Kitulo kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi kwa wananchi wanaozunguka hifadhi hiyo badala ya kutumia nguvu na kuwajeruhi watu.

Alisema kumekuwapo na malalamiko kwa wananchi wanaozunguka hifadhi ya Kitulo kupigwa na askari wa TANAPA bila kupewa nafasi ya kujieleza wanapokutwa maeneo ya hifadhi.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema baada ya mafunzo hayo wataenda kutembelea maeneo yote ya shule zilizonufaika na elimu hiyo kuangalia utekelezaji wa kile walichofundishwa.

Alisema lengo ni kuona matokeo ya elimu hiyo ambayo yanahitaji kuona mabadiliko katika kuhifadhi rasilimali hizo pamoja na kukuza ujirani mwema.





# Mashine zawekwa bandarini kupima joto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeweka mashine maalum katika bandari kupimia joto ili kubaini maradhi ya kuambukiza kwa wasafiri, hivyo kupunguza kuenea kwa maradhi ya kupumua.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalum, Fatma Ramadhan Mandoba, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar.

Swali aliloulizwa waziri huyo lilihusu kutotumika kwa mashine za kupimia joto katika Bandari ya Malindi na uwanja wa ndege wakati serikali imegharamia kununua mashine hizo.

Waziri Mazrui alisema kutokana na miundombinu na ufinyu wa nafasi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Abeid Amani Karume na Bandari ya Malindi, mashine hizo zimekuwa zikiharibika mara kwa mara, hivyo hulazimika kutumika vipima joto vya mkononi ili kufikia lengo lililokusudiwa.

"Kwa mujibu wa taarifa za kitaalamu kutoka kwa mafundi, mashine hizo kuharibika mara kwa mara kunatokana na ukaribu wa eneo zilipo mashine hizo na eneo la nje la uwanja. Mara nyingi mashine huchukua joto la nje ya uwanja na husababisha kupanda sana kwa vipimo vya joto husika," alisema.

Alisema katika kurekebisha hali hiyo, serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na wizara yenye dhamana ya afya inaendelea kuzifanyia marekebisho mashine hizo ili ziendane na hali ya viwanja vya ndege.

Pia alisema hivi karibuni Wizara ya Afya imepeleka mashine zingine mbili mpya za aina hiyo zinazotarajiwa kufungwa katika uwanja wa ndege baada ya kuanza kazi.

Hata hivyo, aliwaeleza wajumbe kufahamu kuwa mashine ndogo za mkono zinazotumika hivi sasa katika viwanja vya ndege na bandari ni kwa ajili ya kupima joto la mwili kwa wasafiri na si kipimo cha corona, kama wanavyofikiria baadhi ya watu. "Hiki ni kipimo kwa ajili ya kujua joto la mwili na msafiri anapogundulika kuwa anajoto la kiwango cha juu ndio hutakiwa kupima kipimo cha corona," alisema Mazrui.

Katika hatua nyingine, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zubeir Ali Maulid, alimwapisha Mwakilishi wa Pandani, Prof. Omar Fakihi Hamad, baada ya kushinda katika uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni.

Mwakilishi huyo kutoka Chama cha ACT-Wazalendo, anachukua nafasi ya aliyekuwa mwakilishi wa jimbo hilo, Abubakar Khamis Bakary, aliyefariki dunia.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na waumini wa dini ya kiislam, baada ya kumalizika kwa Sala ya Tarawekh, katika Masjid Ibadhi, wilayani Wete Pemba juzi. **PICHA: IKULU**

# ZIPA yafanywa kituo kikuu uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema tayari imefanikiwa na kuifanya Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) kuwa kituo kimoja kikuu cha uwekezaji.

Kituo hicho sasa kitashughulikia masuala yote muhimu ya miradi ya uwekezaji Zanzibar, hatua ambayo itapunguza urasimu.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla, alisema hayo jana wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22 katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema serikali imechukua hatua hiyo kwa ajili ya kuleta ufanisi na kushughulikia masuala ya uwekezaji katika miradi mbalimbali kwa haraka na ufanisi wa hali ya juu.

Alizitaja baadhi ya taasisi ambazo zimeunganishwa moja kwa moja na ZIPA katika kuharakisha uwekezaji ni pamoja na Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Taasisi zingine ni Idara ya Uhamiaji, Kamisheni ya Ardhi, Kamati ya Usimamizi wa Ujenzi, Kamisheni ya Mazingira inayoshughulikia na utoaji wa hati za kuthibitisha mradi kupata kibali.

Alisema kuwapo kwa kituo kimoja cha uwekezaji kwa kiasi kikubwa kitapunguza urasimu uliokuwapo wakati huo kwa wawekezaji kuchukua muda mrefu kupata na kukamilisha taratibu mbalimbali katika miradi yao.

Hemed alisema kuwapo kwa kituo kimoja cha uwekezaji kutapunguza urasimu kutoka wiki tatu hadi wiki moja kwa mwekezaji kupata huduma muhimu za kutekeleza miradi yao.

"Nataka niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tayari tumefanikiwa kuunganisha taasisi mbalimbali muhimu za uwekezaji na kufanya kituo kimoja hatua ambayo sasa itaondosha na kupunguza urasimu uliokuwapo awali," alisema.

Alisema katika kufikia mafanikio hayo mamlaka ya uwekezaji nchini (ZIPA) tayari imefanikiwa kuwaka mfumo wa kielektroniki kwa kuziunganisha taasisi zote hizo hatua ambayo itasaidia na kudhibiti mapato ya serikali.

Pia alisema SMZ imejipanga na kukifanya kisiwa cha Pemba kuwa maalumu kwa ajili ya uwekezaji na kazi inayokusudiwa kufanywa kwa sasa ni kuweka miundombinu muhimu ikiwamo majisafi na salama, umeme na barabara za lami ili kuyafikia maeneo ya uwekezaji.

Alisema serikali inakusudia kuifanyia marekebisho Sheria ya Uwekezaji Na. 11 ya mwaka 2018 ambayo itaweka mazingira mazuri na kuondoa kasoro za uwekezaji katika kisiwa cha Pemba.

Serikali, alisema imechukuwa hatua hiyo na kukifanya kisiwa cha Pemba maalumu kwa uwekezaji kwa lengo la kuimarisha uchumi na kutoa ajira kwa wananchi.

Alisema hadi sasa uwekezaji wa miradi ya kiuchumi ikiwamo vitega uchumi kwa upande wa kisiwa cha Pemba haujaimarika vizuri ikiwamo kushindwa kuendelezwa kwa maeneo huru ya kiuchumi Micheweni.

Suleiman alisema tayari serikali imetenga maeneo ya ujenzi wa viwanda vidogo Chamanangwe mkoa wa Kaskazini Pemba kwa ajili ya miradi ya wawekezaji.

## Wakili aongezwa katika kesi vileo

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MWANASHERIA na wakili maarufu Zanzibar, Rajab Abdalla, ameongezwa katika kesi ya kuitetea Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) mahakamani kwenye kesi ya Bodi ya Udhibiti wa Vileo kwa madai ya kuvunja Sheria N. 9 ya Vileo ya Mwaka 2020.

JUMAZA sasa inawakilishwa na mawakili wawili akiwamo Omar Shehe Omar baada ya kesi hiyo kufikia hatua nzito kabla ya kutolewa hukumu Juni 2, mwaka huu mbele ya Jaji wa Mahakama Kuu Zanzibar, Rabia Hussen Mohamed.

Katibu Mtendaji wa JUMAZA, Sheikh Ali Amour, alisema bodi hiyo imeamua kuongeza wakili ili kujenga nguvu ya hoja za kisheria wakati kesi ikiendelea kusikilizwa Mahakama Kuu.

"Tumeona kutokana na uzito wa kesi na mahali ilipofikia, tuongeze wakili kabla ya kesi kutolewa hukumu na Mahakama Kuu. Kesi hii ina umuhimu mkubwa kwa jamii baada ya sheria ya vileo kuvunjwa makusudi na bodi ya vileo," alisema.

Sheikh Amour alisema JUMAZA imefungua kesi Namba 3 ya mwaka 2021 dhidi ya Bodi ya Udhibiti Vileo baada ya kukiuka na kuvunja sheria hiyo.

Kwa mujibu wa hati ya maombi ya malalamiko JUMAZA inadai Bodi hiyo imevunja kifungu cha 33(3) cha sheria baada kutoa vibali kwa kampuni za kuingiza vileo Zanzibar zaidi ya saba badala ya tatu kinyume na taratibu wa sheria.

"Kibali cha kuagiza vileo kinataka kutolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu. Sheria inatamka vigezo kuzingatiwa mwingizaji. Kwanza awe ni Mzanzibari, mlipakodi awe na ghala la kuhifadhia na gari ya kusambazia vileo," kimeeleza kifungu cha 33(3) cha Sheria ya Udhibiti Vileo Zanzibar.

Aidha, JUMAZA wanadai Bodi ya Vileo Zanzibar pia imevunja kifungu cha 28 (K) kinachotaka majengo ya baa yawe umbali wa mita 1,000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama hospitali, nyumba za ibada, shule au makazi ya watu lakini bodi imeshindwa kuyasimamia masharti hayo ya kisheria.

Jaji Rabia alisema kesi itaendelea kusikilizwa kwa maandishi kuanzia Mei 17, mwaka huu kabla ya kutolewa uamuzi Juni 2, mwaka huu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO LA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

DIONIS VISENTHI MASHAURI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA FUSO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 365 BNT YENYE CHASSIS NO FK 615K550011 NA ENGINE NO. 6D14680751 KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/ TR /RB/ 171/2021

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA 14 YA 2021**
**OTEE KIBALENI………………..MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SHABANI MDOE………..MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

SHABANI MDOE Popote ulipo unaarifiwa ufike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 24/05/2021 mbele ya Mh.Khasim wewe mwenyewe binafsi au utume muwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hautahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wang leo tarehe 04 mwezi April 2021

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MOROGORO**

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.125/2021**

Ombi la **SALMINI SELEMAN MSUMI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **SELEMAN ISMAIL MSUMI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 22/06/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe03/05/2021**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL KIKA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0938-0435** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **MBEZI BEACH SEKONDARI** mwaka 2005. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MSI/RB/169391/2021.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.112/2021**

Ombi la **DAUDI MWIJUMA ISSA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **RIDHIWANI MWIJUMA MVUNGI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 17/05/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe05/05/2021**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ENOS SIKAONJA PANJA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 336 AHF – SUZUKI ESCUDO.** Chassis namba **TD01W141823.** Engine namba G16A335431.Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DAR/URA/RB/221953/2021.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GOODLUCK ASAPH MLINGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 122 DRU – NISSAN PATROL.** Chassis namba **JNITESY61Z0575456.** Engine namba **ZD30046048N.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi:
**DAR/CEN/RB/230727/2021.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YA MIGUU MITATU (BAJAJ)

**JOSEPH RUDROF CHAULA** anatangaza kupoteza kadi ya pikipiki ya miguu mitatu **(BAJAJ)** aina yenye namba za usajili **MC.523 CFK** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi
Taarifa ya polisi
***RB. Namba***
**IRI/IRI/RB/230021/2021**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**RICHARD PASCHAL RICHARD** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0108-0114** kilichotolewa na balaza la mitihani kupitia shule ya secondary **IFUNDA TECHNICAL** mwaka 2015,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisis
Polisi taarifa **DAR/MSI/RB/250815/2019**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA )**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**CHAMWINO- DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 02…. 2021**
**Ombi la THEOPHILIDA THEOPHIL MWENDA kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu ROSE THEOPHIL MWENDA .**

Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 06/5/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani Kukaguliwa

……………………………………
**Sahihi ya Hakimu**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya**
**Kituo cha KINGOLWIRA**
**Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 12/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KIBWANA .A. MALINDA WA KINGOLWIRA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ALLY SAID MALINDA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama ya Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 01 mwezi 06 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakama kukaguliwa.
*Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa. *Marehemu hakuacha wosia
Imetolewa leo Tarehe 28 mwezi 4 Mwaka 2021

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi NO.136/2021**
**Ombi la MOHAMED RAMADHANI KAMBI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu RAMADHANI RASHID KAMBI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 07/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe05/05/2021

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi NO.134/2021**
**Ombi la VERDIANA JOSEPHAT MIGEYO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu PASCHAEL RAPHAEL RWEIKIZA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 01/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe05/05/2021

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**RICHARD F RUGAREMA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0397-0056** kilichotolewa na balaza la mitihani kupitia shule ya secondary **RULENGE** mwaka 1994,yeyote atakayekiokot atoe taarifa kituo chohote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/212893/2021**

---

## TANGAZO LA NOTISI KWA WADAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED** inatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku Sitini(60) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa, ikiwemo kukamata na kuuza kwa njia ya mnada dhamana za mikopo kupitia madalali bila taarifa zaidi kwa atakaekiuka tangazo hili.

1. Abiud Alphonce Zagwi- **KIPAWA AIRPORT (Dar)**
2. Chesco Daniel Mpiluka- **Dar es Salaam**
3. Athuman Abdallah Ngajua- **Dar es Salaam**
4. Cyril Michael Wariro **– Dar es Salaam**
5. Magere Mugeta Magere- **LAMADI**
6. Mugeta Magere Mongu- **MAGU**
7. Masasa Makwasa Bwire - **Dar es Salaam**
8. Nazael Eliaza Mungulwi **– Dar es Salaam**
9. David Teu Mbijiri (Petter machege Mokoro) – **Mugumu**
10. Peter Maniyo Phissoo- **MSATA**
11. Steven Buchard Lusangano **– Chanika(Dar)**
12. Omari Said Magoma /Mwajuma Charles Magori.

**Mawasiliano piga: +255 222774742-3/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

---

## K-FINANCE LTD

K-FINANCE Financing . Advisory . Training

MAJEMBE AUCTION MART – TANGAZO LA MNADA WA HADHARA
KWA NIABA YA K-FINANCE LTD TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA GARI LA MDAIWA ANAYETAJWA HAPO CHINI. MAHALI YARD YA MAJEMBE AUCTION MART, DAR ES SALAAM, MBEZI TEMBONI.

| JINA LA MDAIWA | DHAMANA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|
| SAMWEL ZABDIEL TARIMO – ENERGY RORWARDERS LIMITED | GARI AINA YA MERCEDEZ BENZ HEAVY TRUCK NAMBA YA USAJILI T 706 CBW | ALHAMISI 13/05/2021 KUANZIA SAA 5:00 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

1. MNUNUZI ATALIPA HELA YOTE ILIYOFIKIWA KWENYE MNADA
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA UMILIKI NI ZA MNUNUZI
3. KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA SIMU NAMBA

**0715 980025 / 0738 165605 / 0738 165606.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaawa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe 05-05-2021.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMAMOSI tarehe 08-05-2021 kampuni ya LOGISTIC SUB SAHARA itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka MTUKULA kuelekea TUNDUMA kupitia KAHAMA / MOROGORO / MIKUMI. Gari hizo zenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

390 SSC FS / 232 SSC FS UREFU 22.00 UPANA 4.50 KIMO 4.80
T 653 DFA / T 887 DJB

Gari hiyo inatoka MTUKULA kuelekea TUNDUMA kupitia KAHAMA / MOROGORO / MIKUMI. Gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni).

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**MICHAEL DAUDI TESHA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 355 DRZ – TOYOTA PASSO.** Chassis namba KGC1160012432. Kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 680 DRY – TOYOTA LITE ACE.** Chassis namba KM701006233. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/GOG/RB/773639/2020.**

---

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, SEPCO DEBT COLLECTION & AUCTIONEERING CO.** LTD tutauza kwa mnada wa hadhara gari la mdaiwa Sugu, mali ya Ndugu **ABDIEL ALPHONCE MSHANA (TOYOTA LEXUS -T 161 AXF)** - Gari lipo katika yard ya Makumbusho.

Lengo ni kufidia/ kupunguza deni la mkopo analodaiwa. Mnada utafanyika Tarehe 21/05/2021, mahali dhamana ilipo.
Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi.
Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: 0715683777 /0712670704/0713052578 Email: info@sepcoauctioneering.co.tz**

---

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mwanamke ajifungua watoto tisa Mali

**Bamako, MALI**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, Halima Cisse, mwenye umri wa miaka 25, amejifungua watoto tisa, kati yao wa kike watano na wavulana wanne.

Cisse, alijifungua katika hospitali iliyopo ya Morocco Jumanne ambako alikuwa amelazwa.

Waziri wa Mali, Fanta Siby alitoa taarifa hiyo na kwamba mama huyo alijifungua kwa njia ya upasuaji.

Cisse alikuwa akitarajia kijifungua watoto saba, kutokana na uchunguzi wa picha ya skani tumboni ilivyoonyesha.

Uchunguzi huo alifanyiwa nchini Mali na Morocco ingawa haikugundulika amebeba watoto wengine wawili.

Jumanne, Dk. Siby alisema watoto hao na mama yao wanaendelea vyema na wanatarajiwa kurejea nyumbani wiki chache zijazo.

Aliwapongeza madaktari waliomhudumia Mali na Morocco, akisema ujuzi wao ni chanzo cha matokeo mema ya ujauzito huu.

Mimba Cisse, ilishangaza taifa hilo la Afrika Magharibi na iliwavutia baadhi ya wakuu wa nchi hiyo, huku baadhi yao wakisafiri hadi Morocco kwa mazungumzo ya kitaalamu, shirika la habari la Reuters, liliripoti.

Msemaji wa Wizara ya Afya ya Morocco, Rachid Koudhari, aliliambia shirika la habari ya AFP kwamba hakujua uzazi wa aina hiyo hutokea nchini humo.

***BBC***



Mwanahabari akishuhudia namna wafanyakazi wa treni iliyopata ajali na kusababisha vifo zaidi ya 20 na majeruhi 50 juzi, wakiendelea kuliondoa jana, baada ya daraja kukatika kwenye kituo cha Olivos, jijini Mexico. **PICHA: REUTERS**

# Upinzani waunda jeshi jipya Myanmar

**Yangon, MYANMAR**

SERIKALI ya Umoja wa Kitaifa Myanmar, iliyoundwa na upinzani unaoupinga utawala wa kijeshi, umesema umeunda jeshi la ulinzi wa watu, ili kuwalinda wafuasi wao dhidi ya mashambulizi ya jeshi na machafuko yanayofanywa na utawala huo wa kijeshi.

Serikali hiyo ilisema hayo jana kwenye taarifa yake kwamba jeshi hilo jipya lilianza kabla ya Jeshi la Muungano wa Shirikisho na litakuwa na jukumu la kufanya mageuzi muhimu kwenye sekta ya usalama ili kuhitimisha vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyodumu kwa miaka 70. Msemaji wa utawala wa kijeshi hakupatikana kuzungumzia hatua hiyo.

Serikali hiyo iliyoundwa mwezi uliopita na makundi yanayoupinga utawala wa kijeshi, iliahidi kuhitimisha machafuko kurejesha demokrasia.

***DW***

# Mwanahabari atekwa na kundi la jihadi

**Gao, MALI**

SHIRIKA la Waandishi wa Habari Wasi na Mipaka, RSF, limeomba Olivier Dubois, aachiliwe huru mara moja na bila masharti.

Mwanahabari huyo kutoka Ufaransa, alikuwa akifanyia kazi katika mkoa wa Gao, wakati wa alitekwa nyara, lilisema shirika hilo.

Dubois anadai katika video kwamba alitekwa nyara Aprili 8, mwaka huu wakati huo yuko mikononi mwa GSIM, kundi linalodai kutetea Uislamu na Waislamu, linalofungamana na Al-Qaeda.

Katika video hiyo, alitoa wito kwa familia yake, marafiki zake na viongozi wa Ufaransa kusaidia ili aweze kuachiliwa.

"Tuliarifiwa siku mbili baada ya kutoweka kwake," alisema Christophe Deloire kiongozi wa RSF.

"Kwa kushauriana na vyombo vya habari ambavyo vilimwajiri, tumechukua uamuzi wa kutoweka hadharani kisa hiki cha kumteka nyara, ili tusizuie matokeo chanya ya haraka kuhusu kuachiliwa kwake."

"Shirika linaomba hadharani mamlaka nchini Mali na Ufaransa kufanya kila wanachokiweza kusaidia anaachiliwa."

***RFI***

**"Kwa kushauriana na vyombo vya habari ambavyo vilimwajiri, tumechukua uamuzi wa kutoweka hadharani kisa hiki cha kumteka nyara, ili tusizuie matokeo chanya ya haraka kuhusu kuachiliwa kwake."**

# Tshisekedi ateua jeshi kuongoza mikoa miwili

**Kinshasa, DRC**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amefanya uteuzi wa maofisa wa kijeshi, kuchukua usimamizi wa mikoa miwili Mashariki mwa nchi, ili kushughulikia usalama.

Luteni Jenerali Luboya Johnny, ameteuliwa kuwa gavana mpya wa mkoa wa Kivu Kaskazini.

Naibu wake atakuwa Alonga Benjamin huku Luteni Jenerali Constant Kongba akiteuliwa kuwa msimamizi wa mkoa wa Ituri na msaidizi wake, Ekuka Lipopo.

Mwishoni mwa wiki rais huyo alitangaza mikoa hiyo kuwa katika hali ya tahadhari na iliyozingirwa, baada ya msururu wa mauaji yanayotekelezwa na makundi ya wapiganaji wenye silaha.

Rais Tshisekedi aliwataka raia wa nchi hiyo kutoa ushirikiano kwa jeshi na serikali, ili kumaliza tatizo la usalama mashariki mwa nchi.

Akizungumza katika hotuba kwa njia ya televisheni, Rais Tshisekedi alisema hatua ya baadhi ya maeneo ya mashariki mwa nchi kuwa chini ya jeshi ni muhimu, ili kuleta hali ya amani.

Tangu kuingia madarakani mwaka 2019, rais amekua akisisitiza kuwa moja ya azma yake kuu ni kuleta utulivu katika maeneo hayo.

Jimbo la Ituri, limekuwa na vita vya kikabila na jimbo la Kivu Kaskazini huku wapiganaji wa kundi la ADF, wakiwashambulia raia.

Hatua hiyo inamaanisha kuwa wanasiasa wasijihusishe na wanajeshi kwa kuwa walikuwa wanalalamika hawana vifaa tofauti na vile ambavyo wanavipata Umoja wa Mataifa (UN) na kutoa ushirikiano kuwabaini maadui.

Aidha, mashirika ya kiraia yamekuwa yakilalamika kuhusu uhusiano wa wanajeshi wa ngazi za juu kutojali uimarishwaji wa usalama kwa raia.

Iliripotiwa kuwa wapiginaji wenye silaha wamewaua takriban watu 19, wakiwamo wanajeshi kumi baada ya kushambulia vijiji viwili Mashariki mwa DRC.

Rais Tshisekedi alitangaza kwamba mikoa miwili mashariki mwa nchi hiyo, Ituri na Kivu Kaskazini, imezingirwa.

Ongezeko la mashambulizi ya makundi yaliyojihami na machafuko ya kikabila yamesababisha vifo vya watu zaidi ya 300, tangu mwanzoni mwa mwaka huu huku wanajeshi wa serikali na walinda amani wakijaribu kuleta utulivu.

Shambulio la hivi punde lilifanyika siku ya Jumamosi wakati wapiganaji wenye silaha waliposhambulia vijiji viwili katika mji wa Kivu Kaskazini wa Beni, mamlaka za jimbo hilo zilisema.

***BBC***

HABARI MICHEZO

# CONTE AMKARIBISHA MOURINHO SERIE A

**MILAN, Italia**

KOCHA Mkuu wa Inter Milan, Antonio Conte, amemkaribisha Jose Mourinho kwenye Ligi Kuu Italia, baada ya kuteuliwa kuwa kocha mpya wa AS Roma.

Kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Conte, alishawahi kukwaruzana na Mourinho hadharani wakati wote wakiwa kwenye Ligi Kuu England, wakati alipokuwa anainoa Manchester United.

Ilifikia hatua Mourinho alimchukulia Conte kama "mchekeshaji", huku yeye akimuita raia huyo wa Ureno kuwa ni "mtu mdogo".

Hata hivyo, Conte amesisitiza kuwa ana mheshimu kocha huyo wa zamani wa Inter, Mourinho, ambaye anachukua mikoba ya Paulo Fonseca pale Roma kuanzia msimu ujao.

"Ni habari njema kwa kila mmoja, namtakia kila la heri, hasa atakapokutana na Inter," alisema Conte akiiambia Le Iene.

"Kwa uhakika, kuna heshima kati yetu. Naamini atakuwa na wakati bora hapa, hivyo namkaribisha."

Majaliwa ya Conte yamezua shaka licha ya kuiongoza Inter kutwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu Italia tangu Mourinho alipotwaa matatu msimu wa 2009-10.

Mkataba wa sasa wa kocha huyo wa zamani wa Italia na Juventus unamalizika mwaka 2022.

# ALABA KUSAINI MKATABA MADRID



**MUNICH, Ujerumani**

DAVID Alaba anatarajia kusaini mkataba rasmi na Real Madrid wakati wowote mwezi huu, kwa mujibu wa Marca.

Nyota huyo raia wa Austria, amekuwa akihusishwa na uhamisho kwenda klabu kadhaa, wakati mkataba wake wa sasa na Bayern Munich ukiwa mbioni kufika tamati mwisho mwa Juni.

Licha ya klabu kadhaa kuhusishwa na saini ya staa huyu mwenye umri wa miaka 28, kwa mujibu wa mwanahabari Fabrizio Romano, Madrid wamekuwa mbele kwenye mbio hizo tangu Januari.

Taarifa zinasema kuwa, Chelsea, Paris Saint-Germain, Liverpool na Barcelona wameshindwa kumshawishi nyota huyo, huku upande wa kocha Zinedine Zidane ukiwa na nafasi nzuri zaidi.

Alaba anatajwa kuwa anatarajia kusaini mkataba na Real Madrid wakati wowote kuanzia sasa, na anaonekana ataweza kuziba pengo la Sergio Ramos, ambaye hadi sasa bado hajakubali kusaini mkataba mwingine pale Bernabeu.

Alaba, kwa mara nyingine amekuwa mchezaji muhimu sana kwenye kikosi cha Bayern msimu huu, akifunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho tano kwenye mechi 42 alizocheza za michuano yote.



# KROOS:

## NAAMINI ZIDANE ATABAKI REAL MADRID

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa Real Madrid, Toni Kroos, anatarajia Kocha Mkuu, Zinedine Zidane, atabaki klabuni hapo baada ya msimu huu.

Baada ya kushinda LaLiga msimu uliopita, Madrid ipo pia kwenye mbio za kuwania taji hilo msimu huu, wakiwa wamepitwa pointi mbili na vinara Atletico Madrid, huku zikiwa zimebaki mechi nne LaLiga kufikia mwisho.

Akizungumza kabla ya mchezo wa jana Jumatano wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wa Madrid na Chelsea, baada ya mchezo wa kwanza kutoka sare ya 1-1, Kroos aliulizwa kuhusu Zidane.

"Nafikiri atakuwa kocha wetu msimu ujao," alisema Kroos wakati akizungumza na waandishi wa habari huku akicheka.

"Bado ana mkataba na Madrid, na nina amini kuwa kuna uwezekano wa yeye kuendelea kuwapo hapa msimu ujao.

Majaliwa ya Zidane pale Madrid yameibuka mjadala na kwa mujibu wa ripoti kuna uwezekano asiendelee kuwa kocha wa kikosi hicho msimu ujao.

## MARTINEZ KUONDOKA BAYERN MSIMU HUU

**BAYERN, Ujerumani**

JAVI Martinez ataondoka Bayern Munich mwishoni mwa msimu huu, mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, wamethibitisha.

Martinez alijiunga na Bayern akitokea Athletic Bilbao mwaka 2012 kwa dau la pauni milioni 40 na mara moja alilipa kile ambacho kilikuwa kikitarajiwa na klabu hiyo.

Endapo Bayern itakamilisha taratibu za kushinda taji la tisa mfululizo la Bundesliga - ambalo kwa uwezekano wote litakamilika wikendi hii inayokuja - Martinez atakuwa mchezaji pekee katika historia ya Bundesliga kushinda mataji tisa.

Thomas Muller, Manuel Neuer, David Alaba na Jerome Boateng pia wamekuwa sehemu ya mafanikio yote tisa mfululizo.

Lakini Alaba na Boateng watajiunga na Martinez na kocha mkuu Hansi Flick kuondoka Bayern mwishoni mwa msimu huu.

Licha ya kusumbuliwa mara kwa mara na majeraha wakati akiwa pale Allianz Arena, Martinez ameichezea Bayern mechi 266, akifunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho 11.

"Ninajivunia sana na nimefurahi kuwa sehemu ya familia ya FC Bayern kwa miaka tisa. Ningependa kuishukuru klabu hii na haswa mashabiki wetu ambao wamenifanya nijisikie kama niko nyumbani," mchezaji huyo wa miaka 32, akiiambia tovuti ya Bayern.





# GATTUSO
## ATAFUTIWA MBADALA NAPOLI

**NAPLES, Italia**

KLABU ya Napoli inafikiria uwezekano wa kumbadilisha Gennaro Gattuso na imeandaa orodha ya makocha watatu, kwa mujibu wa Sky Sport Italia.

Taarifa zinafafanua Napoli tayari imeanza kupanga uwezekano wa kuishi bila uongozi wa Gattuso.

Inaonekana ni ngumu kwa Gattuso kuendelea kuwapo hapo kwenye dimba la Diego Maradona, hata kama Napoli ingefuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ripoti hiyo inadai Rais Aurelio De Laurentiis, tayari ameandaa orodha ya wanaoweza kuchukua nafasi hiyo, huku pia jina la Luciano Spalletti likiwapo kwenye orodha hiyo.

Kocha huyo wa zamani wa Inter na Roma ametajwa kuwapo kwenye mazungumzo na klabu hiyo katika wiki za hivi karibuni.

Kocha wa Lille, Christophe Galtier, pia anatajwa na Sky Sport Italia kama miongoni mwa wanaodhaniwa kufaa kwenye nafasi hiyo.

Jina la mwisho kwenye orodha ni Vincenzo Italiano, ambaye ameisaidia Spezia kupanda Serie A.

Ripoti zinaeleza kuwa uhusiano kati ya Gattuso na De Laurentiis haupo kwenye wakati mzuri.

## EURO 2020 KILA TIMU NA WACHEZAJI 26

**NYON, Uswisi**

SHIRIKISHO la Soka Ulaya (UEFA), limethibitisha kwamba, timu zinazoshiriki mashindano ya Euro 2020 yaliyocheleweshwa mwaka huu, zitaruhusiwa kuchagua kikosi cha wachezaji 26 badala ya 23 kama ilivyokuwa hapo mwanzo.

Mabadiliko hayo yametolewa ili kupunguza mzigo kwa wachezaji kufuatia msimu ulioshinikizwa wa klabu na kuzisaidia timu za taifa wakati huu wa mlipuko wa virusi vya corona.

Kamati Kuu ya UEFA iliidhinisha pendekezo hilo Jumanne na ilitangaza timu zinaweza kufanya mabadiliko bila kikomo kwenye kikosi chao. Kanuni mpya pia zitaruhusu magolikipa kubadilishwa kabla ya kila mechi, hata kama walinzi wengine wawili kutoka orodha ya kwanza bado wanapatikana.

Lakini sasa timu zinaweza kutaja vikosi vya watu 26, ni 23 tu kati ya hao wanaweza kuchaguliwa kwa siku ya mechi.

Bosi wa Ubelgiji, Roberto Martinez (pichani) na Roberto Mancini wa Italia ni miongoni mwa wale ambao walitaka ukubwa wa kikosi uongezwe.

UEFA ilithibitisha Machi kwamba, timu zinaweza kufanya mabadiliko mpaka mara tano kwa kila mechi, badala ya tatu za kawaida.

Mashindano hayo, yaliyocheleweshwa kwa mwaka kwa sababu ya janga la corona, yataanza Juni 11, mwaka huu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MAHREZ SASA SHUJAA WA GUARDIOLA CITY

**Ana kipaji kikubwa, ubora wa hali ya juu, hasa kwenye mechi kubwa anaweza kuamua matokeo...**

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amepaza sauti kwa Riyad Mahrez na kumsifia winga huyo wa Manchester City aliyefunga mabao mawili na kuwezesha ushindi wa 2-0 dhidi ya Paris Saint-Germain na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Shuti la adhabu ndogo la Mahrez wiki iliyopita pia lilipa ushindi wa 2-1 pale katika dimba la Parc des Princes wiki iliyopita na juzi Jumanne alifunga bao katika kila kipindi na kuiwezesha kutinga fainali kwa ushindi wa uwiano mabao 4-1.

> Nyota huyo wa zamani wa Leicester City alikuwa akikabiliwa na wakati mgumu tangu alipojiunga a na City mwaka 2018 , lakini sasa amekuwa chaguo la kwanza kwa Guardiola, akifikisha bao la nne na pasi mbili za mwisho kwa msimu huu.

"Riyad ni mchezaji wa aina yake - kipaji kikubwa, ubora wa hali ya juu, hasa kwenye mechi kubwa na mara zote yupo tayari," alisema kocha wa City, Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunajua ubora wake vizuri. Ni mchezaji wa kuvutia.

"Wachezaji kama yeye wanakuwa na wakati bora wa kuamua matokeo kwenye mechi kubwa.

"Anapenda na kufurahia. Alitengeneza bao zuri, la kwanza kwa mguu wa kulia na akamaliza kwa bao la pili. Mabao haya yalikuwa muhimu na alistahili."

Man City sasa watacheza fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Chelsea au Real Madrid ambao walikuwa wakicheza jana kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali.

Katika mchezo wa kwanza, timu hizo zilitoka sare ya kufungana bao 1-1.

## KWA UFUPI

**STERLING AWANIWA MADRID**
REAL Madrid wanamfuatilia mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 26, ambaye anaweza kuondoka Etihad kwa kitita cha pauni milioni 75. (**Football Insider**)

**ANCELOTTI AMWANIA BALE**
KOCHA wa Everton, Carlo Ancelotti, anataka kumsajili mshambuliaji wa Real Madrid, Gareth Bale mwenye umri wa miaka 31, anayecheza kwa mkopo Tottenham Hotspur msimu huu. (**El Chiringuito, via Sport Witness**)

**JOHNSTONE KUMRITHI DE GEA**
KLABU ya Manchester United imejiunga na Tottenham Hotspur na West Ham katika kinyang'anyiro cha kumsajili mlindamlango wa West Brom, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28, ikijiandaa kuondoka kwa David de Gea mwenye umri wa miaka 30, msimu huu wa joto. (**ESPN**)

**DORTMUND KUMUUZA SANCHO**
BORUSSIA Dortmund itahitaji pauni milioni 85 kwa ajili ya kumwachia Jadon Sancho wakati wa kipindi cha majira ya joto, kiasi ambacho bado ni zaidi ya kile ambacho Manchester United iko tayari kulipa. (**Eurosport**)

**HEATON AWANIWA UNITED**
MANCHESTER United pia itamfuatilia mlinda mlango wa Aston Villa, Tom Heaton mwenye umri wa miaka 35, kama Sam Johnstone atapendelea kwenda West Ham.(**Star**)

**CAMPBELL ATAKA UKOCHA**
MLINZI wa zamani wa England, Sol Campbell mwenye umri wa miaka 46, ni miongoni mwa walioomba nafasi ya kuwa mbadala wa kocha Aidy Boothroyd katika nafasi ya ukocha wa timu ya Taifa ya England chini ya umri wa miaka 21.(**Mail**)

**SANCHO AGOMBEWA EPL**
CHELSEA wanaweza kujiunga na Manchester United na Liverpool kuwania saini ya winga, Jadon Sancho baada ya Borussia Dortmund kushusha dau la kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka miaka 21. (**Bild, via Football London**)

**LEEDS YAMWANIA LANG**
LEEDS United wanafikiria kumsajili winga wa Club Bruge, Noa Lang raia wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 21. (**Telegraph**)

**LUIZ ATAFUTA TIMU**
WAKATI David Luiz mwenye umri wa miaka 34, anaingia miezi miwili ya mwisho ya mkataba wake na Arsenal, wawakilishi wake wameanza kutafuta klabu mpya kwa ajili ya Mbrazil huyo. (**CBS Sports**)

**BUENDIA SASA LULU ULAYA**
KIUNGO wa kati wa Norwich City, Emi Buendia mwenye umri wa miaka 24 anatolewa macho kwa kiasi kikubwa na klabu za Arsenal, Aston Villa, Crystal Palace, Atletico Madrid, Sevilla na Villareal. (**Footmercato**)

**BEI YA JOHNSTONE YATAJWA**
KLABU ya West Brom inataka kiasi cha pauni milioni 20 kwa ajili kumwachia Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28. (**Telegraph**)

HABARI MICHEZO

# SIMBA YA GOMES YA SVEN MTOTO - MANARA

**Na Adam Fungamwango**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi Jumamosi kati ya Simba na Yanga, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Haji Manara, amesema soka linalochezwa na wachezaji chini ya kocha wa sasa, Mfaransa Didier Gomes da Rosa, ni zaidi ya lile lililokuwa likichezwa ilipokuwa chini ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Manara alisema chini ya Mfaransa huyo, Simba imekuwa ikicheza kandanda lenye malengo, lakini likiwa kwenye falsafa ile ile ya soka la chini, pasi fupi, kasi na safari hii likiongezewa umakini pamoja na kujitoa kwa wachezaji.

Alisema wakati wa Mbelgiji Sven, Simba ilikuwa ikicheza soka la pasi nyingi, lakini zilikuwa zikipigwa bila malengo na ilionekana kama ni za kufurahisha mashabiki zaidi.

"Simba ya sasa, inapiga kweli pasi nyingi fupi fupi, lakini wachezaji wakishavuka mstari wa kati wanaongeza spidi na hata mpira unaweza kupigwa kutoka upande huu kwenda mwingine, ikionekana kabisa kuwa goli linatafutwa. Wakati wa Sven timu haikuwa na kasi. Pasi zinapigwa hadi ndani ya eneo la 18, lakini wachezaji bado wako taratibu sana," alisema Manara.

Alisema kilichoongezeka kingine ni wachezaji wote wa Simba kukaba na jukumu hilo ni la wote, kitu ambacho si Sven tu, hata makocha waliopita walikuwa na tatizo hilo.

"Kuna siku nilikuwa naangalia mechi pale, nikamwambia kiongozi mmoja wa Simba, hivi mnashangilia nini sasa hapa. Mbona hizi pasi hazina maana yoyote. Hatushambulii wala hatuonyesha kama tunatafuta bao, hiyo ilikuwa ni wakati wa Sven, lakini kwa sasa timu ikiamua kushambulia ni balaa, inashambulia kwa nguvu na kasi kubwa," alisema.

Sven aliondoka klabuni hapo Januari mwaka huu baada ya kuiwezesha Simba kuingia hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku Gomes akirithi mikoba hiyo, naye akifanikiwa kuipeleka timu hiyo kileleni mwa Ligi Kuu Tanzania Bara na kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiongoza kwenye Kundi A lililokuwa likiundwa na mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo pamoja na Al-Merrikh ya Sudan.

WAYAAA...



Winga wa Manchester City, Mualgeria Riyad Mahrez (Jezi Na. 26), akiifungia timu yake moja kati ya mabao mawili aliyofunga wakati wakiibuka na ushindi wa 2-0 dhidi ya PSG kwenye nusu fainali ya mkondo wa pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi, hivyo kutinga fainali kwa jumla ya mabao 4-1 kutokana na mechi ya awali ugenini kushinda 2-1. **HABARI UK. 22**

## Azam FC wafukuza mwizi kimyakimya Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, amesema wanapambana kushinda mechi zao bila kuwaangalia waliopo juu yao, Simba na Yanga, ambao kwa pamoja wako katika vita vya kugombea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, Vivier alisema hawana muda wa kupoteza kuwaangalia wapinzani wao na badala yake wanaendelea na mazoezi ili kuweza kupambania ubingwa.

Alisema licha ya kuwapo kwa ugumu katika michezo iliyopo mbele yao ya ligi, wanapambana kuhakikisha wanaandaa vikosi kutafuta matokeo chanya kila mechi ikiwamo dhidi ya KMC FC.

"Tumepata pointi tatu kwa Yanga, tumeweza kupunguza idadi kwao, lakini kuhakikisha tunashinda mechi zilizopo mbele yetu na sasa tunajiandaa kwa ajili mchezo dhidi ya KMC FC, walitufunga mechi ya kwanza sasa hatutakubali kupoteza.

"Hakuna kisichowezekana ukizingatia Yanga ambayo iko nafasi ya pili, tumepishana nao pointi tatu sawa na mechi moja tukishinda, na Simba iliyopo kileleni ametupita pointi saba kwa mechi tatu tu tupate ushindi jambo ambalo linawezekana," alisema kocha huyo.

Alisema anatambua ugumu uliopo kwenye ligi hiyo, lakini wao wanapambana kushinda mechi zao huku wakiwaombea mabaya wapinzani wao hao.

Azam FC iko nafasi ya tatu ikiwa na pointi 54, ikicheza michezo 28, wakati iliyopo nafasi ya pili baada ya mechi 27 ina pointi 57, nne nyuma ya vinara Simba walioshuka dimbani mara 25.

## Simba, Yanga SC zaburuzwa Ligi U-20

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba, Yanga na Azam zikitamba kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, vikosi vya pili vya timu hizo vinaonekana kuburuzwa kwenye Ligi ya Vijana chini ya miaka 20 ambayo inazishirikisha vikosi vya timu zote zinazocheza ligi.

Simba kubwa inaongoza kwenye Ligi Kuu ikiwa na pointi 61, lakini timu yake ya vijana U-20 inashika nafasi ya pili kwenye Kundi B chini ya Mtibwa Sugar ambayo inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 16.

Timu za Prisons, Mbeya City na KMC zinafuatia huku timu ya Ihefu ikishika mkia ikiwa na pointi mbili, timu zote zikicheza mechi saba.

Katika ligi hiyo ya vijana, inachezwa kwenye makundi matatu, A, B na C, kila kundi likiwa na timu sita ambapo Ruvu Shooting, ndiyo inayoongoza Kundi A linaloonekana kama ni kundi la kifo ikiwa na pointi 11, ikifuatiwa na Yanga ambayo nayo ina pointi 11 na Azam FC inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi kama hizo, zote zikitofautiana mabao ya kufunga na kufungwa.

## Gwambina mafichoni kutafuta alama saba

**Na Saada Akida**


KOCHA Mkuu wa timu ya Gwambina FC, Mohammed Badru, amesema malengo yake makubwa ni kuhakikisha anainusuru timu hiyo kutoshuka daraja na moja ya mikakati yake ni kushinda mechi tatu, mbili akicheza nyumbani na moja ugenini kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mechi zijazo za Gwambina FC ambazo inazipigia hesabu hizo ni dhidi ya JKT Tanzania itakayopigwa Mei 14, mwaka huu, kabla ya siku tano baadaye kuikaribisha Namungo FC (mchezo wa kiporo) katika Uwanja wa Gwambina na kisha kuifuata tena timu hiyo kwenye dimba la Majaliwa mkoani Lindi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Badru alisema wako katika nafasi ya 12 ambayo si salama kwao kutokana na ugumu wa ligi hiyo, hivyo anapaswa kuhakikisha anaendelea kuwapa mbinu na majukumu wachezaji wake ili kupambana kutafuta pointi hizo saba katika michezo hiyo mitatu.

"Ni mechi ngumu sana kwa pande zote, kwa sababu tunafahamiana vizuri na kati yetu tuliwahi kukutana tukiwa na timu mbalimbali huko Zanzibar, lakini kwa upande wangu napambana kutafuta pointi zote sita nyumbani na ikiwezekana tatu au mmoja ugenini," alisema Badru.

Michezo
Alhamisi Mei 6, 2021
Nipashe



MAHREZ SASA SHUJAA WA GUARDIOLA CITY

HABARI UK 22




Beki wa kati wa Simba, Joash Onyango (Kushoto) na wa Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja', wakiwania mpira kwa kichwa kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar iliyopigwa katika Uwanja wa Karume visiwani humo Januari 13, mwaka huu na kumalizika kwa sare tasa ndani ya dakika 90 kabla ya Yanga kushinda kwa mikwaju ya penalti 4-3. Mtifuano kama huo unatarajiwa kushuhudiwa tena Jumamosi katika mechi ya Ligi Kuu itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA YETU**

# GOMES: HESABU KAIZER CHIEFS CAF KWA YANGA

●●●Asema wana kila sababu ya kushinda Jumamosi, uongozi wadai haki ikitendeka uwanjani, hatoki mtu kwani...

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya kukabiliwa na kibarua kigumu Mei 14, mwaka huu kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika ugenini dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, amesema wanaweza kurahisisha kazi hiyo kwa kupata ushindi Jumamosi dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga.

Simba yenye pointi 61 kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara baada ya kushuka dimbani mara 25, itakuwa mwenyeji wa mechi hiyo dhidi ya Yanga inayoshika nafasi ya pili na alama zake 57 zilizotokana na michezo 27.

Lakini wakati huu, mashabiki wa timu hiyo wakiwaza mechi hizo mbili dhidi ya Yanga na baadaye Kaizer Chiefs, Gomes amesema endapo watashinda Jumamosi, itakuwa rahisi kwao kupata matokeo chanya kwenye mechi hiyo ya CAF.

"Kama tukiwafunga Yanga, ni wazi tutakwenda kukutana na Kaizer tukiwa vizuri, ndio maana tumedhamiria kulifanya hilo, na kutokana na wachezaji wangu walivyo inawezekana," alisema Gomes.

Hata hivyo, wakati Gomes akipiga hesabu ya kutumia jiwe la kuiua Yanga kwenda kuimaliza Kaizer Chiefs, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Haji Manara, amesema kwa ubora wa kikosi chao na morali iliyopo kwa wachezaji, wanaamini kama refa atachezesha kwa haki hakuna kitakachowazuia kuibuka na ushindi.

Manara alisema siku zote morali ya Yanga ni kucheza kwa jitihadi sambamba na rafu na fujo nyingi, jambo ambalo mwamuzi anapaswa kuwa makini na kutofumbia macho kwa kuhofia kutoa kadi kwa wachezaji watakaocheza rafu iwe wa Yanga ama wa Simba.

"Hatumpi shinikizo refa ila haki itendeke, mtu anapocheza rafu kama ni kadi nyekundu au ya njano mpe, unajua kuna lugha wanazungumza Simba ukitaka kuwaweze wewe wagonge tu.

"Mechi ya mwisho kama refa angekuwa makini kungekuwa na red kadi ngapi? Wote mnaikumbuka ile mechi, hatutoi shinikizo ila mtu akicheza rafu iwe Simba ama Yanga kadi zitoke tu," Manara alisema.

Alisema wanataka kuona mechi ikimalizika hakuna majeruhi kwa kuwa mpira ni kupasiana si kugongana, na hilo lisiwaingie akilini wachezaji wa Yanga kwamba ukitaka kucheza na Simba dawa ni kuwagonga.

"Hatutarajii kuona wachezaji wetu wakitoka na majeraha kwa sababu tu ya uwezo wao mkubwa. Katika mpira wa kisasa timu nzuri inapaswa kushinda, ile dhana ya Simba nzuri inaweza kufungwa na Yanga mbovu hiyo kwa sasa haipo," alisema.

Manara alisema, "kikubwa ni waamuzi kuchezesha kwa haki bila mambo mengine, na kama kuna mtu anacheza rafu zikitoka kadi za njano kwa wachezaji wawili, mpira utatulia na watu watacheza mpira".

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), waamuzi watakaosimamia mchezo huu ni mwamuzi wa kati Emmanuel Mwandembwa kutoka Arusha huku wa akiba akiwa ni Ramadhani Kayoko wa Dar es Salaam. Waamuzi wa pembeni, namba moja ni Frank Komba kutoka Dar es Salaam na namba mbili akiwa ni Hamdani Said wa Mtwara.

## NABI ANA JAMBO LAKE JUMAMOSI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amewafungia kazi watani wao wa jadi, Simba, kwa kuwapa majukumu muhimu washambuliaji wake kuelekea mchezo huo wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga ambayo imeweka kambi Avic Town, Kigamboni, huku ikifanya mazoezi jioni badala ya asubuhi kama ilivyokuwa awali, Nabi ameelekeza nguvu na ujuzi wake katika kuinoa safu ya ushambuliaji ikiongozwa na Saidi Ntibazonkiza.

**Nabi amesema hiyo itakuwa ni mechi yake ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara tangu alipokabidhiwa majukumu ya kukinoa kikosi cha timu hiyo, akipoteza dhidi ya Azam FC, lakini ikiwa ya tatu kwa ujumla wake baada ya kushinda dhidi ya Tanzania Prisons ugenini kwenye mchezo wa hatua 16-bora ya Kombe la FA.**

Akizungumzia mchezo huo dhidi ya Simba, Nabi amesema wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya mechi zao zilizobaki ukiwamo huo watani wa jadi kufanya vizuri na kufikia malengo yanayotarajiwa.

"Tupo tayari kwa ajili ya mechi zetu zijazo na tunahitaji kupata ushindi kwani kila kitu kipo sawa na maandalizi yanaendelea vizuri, mechi yetu ijayo itakuwa na ushindani mkubwa na tumejipanga kuhakikisha tunaenda kupambana na kutafuta matokeo chanya katika mchezo huo," alisema Nabi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002